JACKPOT BABA LAO!
TZS.374,935,160
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



RIPOTI MAALUM -2
**Watelekeza** familia kisa ukosefu wa samaki bwawani
UKURASA 4




UKURASA 9


# Nipashe JUMAPILI

MWANGA WA JAMII

Jumapili Oktoba 30, 2022 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • No. 0581114

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US




# Polisi wapeleka madereva wodini

• **Ni** waliko majeruhi wa ajali, wataka wajue athari za uzembe wao... *Endelea ukurasa 2*



Rais Samia Suluhu Hassan, akizungumza na Rais wa Kampuni ya TotalEnergies katika masuala ya Utafiti na Uzalishaji, Nicolas Terraz, baada ya kuwasili pamoja na ujumbe wake, Ikulu Chamwino, mkoani Dodoma jana. **PICHA: IKULU**

## Wazee waliopotoka kimaadili wamchefua waziri

UKURASA 2



## ACT Wazalendo yaja na mapendekezo manne uhaba wa maji nchini

UKURASA 8

MICHEZO SIMBA QUEENS KARATA YA KWANZA LEO UK.24

KATUNI UK.6

# Madereva wapelekwa wodi za majeruhi ajali

**Na Friday Simbaya,** IRINGA

KIKOSI cha Usalama Barabarani Mkoa wa Iringa kimewapeleka madereva wa mabasi makubwa waliokamatwa kwa makosa mbalimbali ya usalama barabarani, wodi za majeruhi wa ajali kuona namna wanavyoteseka kutokana na uzembe unaofanywa na baadhi yao.

Madereva hao ni wale waliokamatwa na wengine kufutiwa leseni kwa makosa mbalimbali ikiwamo kuendesha kwa mwendo kasi.

Akizungumza na Nipashe jana ofisini kwake, Mkuu wa Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani Mkoa wa Iringa, Mosi Ndozero alisema wamefanya hivyo ili madereva hao wajionee namna majeruhi wanavyoteseka kutokana na ajali za barabarani.

Alisema madereva hao waliwapeleka juzi wodi za wanawake na wanaume katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Iringa ikiwa ni sehemu ya mafunzo ya siku mbili yaliyoandaliwa kwa kundi hilo.

Ndozero alisema ziara ya madereva hao wodini ambapo kati yao, 12 wamefutiwa leseni kwa makosa mbalimbali, ni mwendelezo wa kutoa elimu na mafunzo ya udereva wa kujihami ili kupambana na ajali.

Daktari wa Kitengo cha Upasuaji katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Iringa, Idd Omary alisema kama madereva wakizingatia sheria za barabarani, watapunguza vifo vingi, majeruhi na watu kupoteza viungo kwa sababu ya ajali.

"Hali ni mbaya na ajali nyingi zinaepukika, kama mnavyoona wagonjwa hawa, wengi ni kwa sababu ya ajali za barabarani," alisema.

Dereva wa kampuni ya mabasi ya New Force, Ambrose Lyimo alisema mafunzo hayo yamembadilisha na amekiomba kikosi hicho kiendelee kuyatoa kwa wenzao ambao hawajanufaika nayo.



Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, akizungumza jijini Arusha juzi, wakati wa harambee ya kuchangia fedha kwa ajili ya ufunguzi wa ofisi za baraza mahususi kwa wazee wanaume katika mikoa yote nchini. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# Waziri ageukia wazee waliopotoka kimaadili

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima amesema zama hizi wanahitaji wazee wafanye mengi ili kuambukiza vizazi vipya tabia njema, lakini baadhi yao wanaripotiwa kufanya matukio ya ajabu yasiyolingana na umri wao.

Akizindua harambee ya kuchangia Chama cha Wanaume Wazee Tanzania iliyofanyika jijini Arusha juzi, Waziri Gwajima alisema wazee ambao ni viongozi wa familia wana nafasi kubwa katika maadili ya vijana.

"Katika zama hizi tunahitaji zaidi wazee waendelee kufanya mengi ili kuambukiza vizazi vipya tabia njema na kuwezesha nao kufikia uzee ulio mwema.

"Cha kusikitisha hivi karibuni kumekuwa na baadhi ya wazee wanaoripotiwa kufanya matukio ya ajabu yasiyolingana na umri wao, mfano kubaka na kulawiti watoto, kuozesha watoto wadogo na kupandikiza imani mbaya," alisema.

Kutokana na mmomonyoko wa maadili kushamiri ndani ya jamii, Waziri Gwajima alisema wazee wanatakiwa kuhakikisha wanawalea vijana kwa ajili ya maisha yao ya uzeeni.

Waziri huyo alisema wazee wana nafasi kubwa ya kukemea vitendo vyovyote ambavyo ni kinyume cha maadili ya jamii ya Kitanzania.

"Kwa sasa tunapita katika kipindi cha mmomonyoko wa maadili ndani ya jamii, hili ni changamoto na wazee tusiposimama vizuri kwa nafasi yetu kubeba ulezi wa jamii, tutajikuta tunapata wazee wa kesho na keshokutwa ambao watashindwa kulea vizazi vinavyokuja," alionya.

Waziri Gwajima alisema chombo hicho kina ulazima wa kuwa na jukumu la kujua kinafanya nini ili maadili ya vijana yaendelee kuwa mazuri kwa manufaa ya kizazi kijacho.

Pia alikitaka chama hicho kushirikiana kwa karibu na Baraza la Ushauri la Wazee na serikali katika kutekeleza afua mbalimbali kwa ustawi wa wazee.

Katika uzinduzi huo, kiongozi huyo alieleza juhudi za serikali zinazofanywa kuhakikisha ustawi wa wazee ikiwamo kuimarisha mifumo, ili wazee wapate huduma za kijamii kama afya, ulinzi, usalama na matunzo kwenye makazi ya wazee.

Kiongozi Mkuu wa chama hicho, Tadey Mchena alisema wanakusudia kupata Sh. milioni 100 kwa lengo la kununua kiwanja kwa ajili ya ujenzi wa ofisi ya Makao Makuu ya chama, kuelimisha jamii, kuwasaidia wazee bima ya afya na vitendea kazi.

Katibu Mkuu wa chama hicho, John Sagata alisema wana malengo ya kuwasaidia wazee katika masuala mbalimbali ikiwamo matibabu kupitia bima ya afya.

Katika harambee hiyo zilikusanywa Sh. milioni 30, ahadi ikiwa Sh. milioni 11 na fedha taslimu Sh. milioni 19 huku Waziri Gwajima akichangia Sh. milioni mbili.

# Vifo vitokanavyo na kemikali vyaongezeka

**Na Mary Geofrey**

IDADI ya vifo vitokanavyo na matumizi ya kemikali zenye madhara kiafya na kimazingira inazidi kuongezeka, Mkemia Mkuu wa Serikali amebainisha.

Kutokana na hali hiyo, jitihada za makusudi zinahitajika katika kutoa elimu ya kutosha kuepukana na madhara yatokanayo na kemikali hizo nchini.

Mkemia Mkuu wa Serikali, Dk. Fidelice Mafumiko alibainisha hayo juzi jijini Dar es Salaam wakati akifunga mafunzo ya siku mbili yaliyoandaliwa na Shirika la Umoja wa Mataifa linalohusika na utafiti kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali.

Alisema idadi ya vifo vitokanavyo na matumizi ya kemikali hatarishi hadi kufika mwaka 2019 ilifika milioni mbili na itaongezeka kama haitaendelea kutolewa.

Dk. Mafumiko alisema mafunzo hayo yaliwakutanisha wataalamu wa serikali na sekta binafsi kujadili kwa pamoja na kuwa na uelewa mpana wa namna ya kuepukana na matumizi ya kemikali hatarishi kwa binadamu na mazingira.

"Ofisi yangu imeshirikiana na shirika la Umoja wa Mataifa linalohusiana na utafiti kufanya mafunzo haya ya mfumo wa kidunia wa kufuatilia usafirishaji wa kemikali kutoka zinapozalishwa hadi kwa watumiaji pamoja na kuwa na alama za utambuzi wa kemikali hizo ili kuepukana na madhara yatokanayo na kemikali hizo ikiwamo vifo," alisema Dk. Mafumiko.

Ofisa Sera Mazingira ya Biashara kutoka Shirikisho la Viwanda nchini (CTI), Anna Kimaro alisema mafunzo hayo yatawasaidia kuchukua tahadhari dhidi ya matumizi ya kemikali hatarishi kwenye maeneo yao ya kazi.

"Wanachama wetu ndio watumiaji wakubwa wa kemikali, mafunzo haya yatatusaidia kuondoa madhara ya kemikali kwenye viwanda na kuweka alama za utambuzi wa kemikali hizo," alisema Anna.

## HABARI KITAIFA

# Waziri ahimiza usomaji vitabu

**Na Beatrice Shayo**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Jenista Mhagama amewataka Watanzania kujijengea utamaduni wa kusoma vitabu ili kuwa na taifa lenye watu waliojielimisha.

Mhagama alitoa rai hiyo juzi jijini Dar es Salaam wakati wa uzinduzi wa maktaba ya uongozi iliyoanzishwa na Taasisi ya Uongozi kwa lengo la kuhifadhi kumbukumbu za viongozi.

Pia kilizinduliwa kitabu cha Hayati Benjamin Mkapa cha 'My Life My Purpose' (Kusudio la Maisha Yangu) kilichotafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili.

"Ninatoa rai kwa Watanzania wote, tuongeze kasi ya kusoma vitabu ili tujenge taifa ambalo limejielimisha lakini pia kujenga ushawishi wa mtu mmoja mmoja kumshawishi mwingine. Vitabu vinasaidia kuongeza maarifa kwa wabobezi katika shughuli tunazozifanya," alisema.

Waziri huyo pia alisema kuna umuhimu wa kuwa na machapisho yanayoendana na wakati huu wa sayansi na teknolojia, hivyo wadau wajitahidi kujenga maktaba.

Vilevile aliwahimiza viongozi wa serikali na viongozi wa vyama vya upinzani kuandika tawasifu zao ili kueleza shughuli walizozifanya katika maisha yao kwa lugha ya Kiswahili ili Watanzania wengi wavisome.

Awali, Kiongozi wa ACT Wazalendo, Zitto Kabwe alisema kuna haja kuondoa kodi kwenye vifaa vyote vinavyohusisha vitu vya kusoma ikiwamo magazeti, karatasi za kuchapisha magazeti na vitabu pamoja na wino.

Mbunge wa Ubungo (CCM), Prof. Kitila Mkumbo alisema kuna haja ya kufufuliwa maktaba za jamii ili kuwawezesha wanafunzi kujisomea kwa wakati. "Kinachotakiwa ni kujenga jamii yenye kupenda mawazo mbadala, turuhusu majadiliano kuanzia shuleni na vyuoni. Majadiliano haya yatamlazimisha mtu kusoma tu. Viongozi wetu watengeneze mazingira mazuri ya kujadiliana," alisema.

Prof. Saida Yahya Othman alisema wazazi wanapaswa wawajengee watoto wao utamaduni wa kusoma vitabu badala ya kuwanunulia simu.



Wafanyakazi wa kiwanda cha kuchakata vyuma Chilambo General Co. Ltd, wakiteketeza sehemu ya mashine haramu za kamari 'slots machine' 300, zilizokamatwa na Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania (GBT), katika mikoa mbalimbali nchini, kiwandani hapo, wilayani Kisarawe, mkoani Pwani juzi. **PICHA: HALFANI CHUSI**

# Mashine 300 za kamari zateketezwa kwa moto

**Na Halfani Chusi**

BODI ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania (GBT) imeteketeza jumla ya mashine haramu 300 za michezo hiyo zenye thamani ya Sh. milioni 300.

Uteketezaji huo ulifanyika juzi katika Kiwanda cha Chilambo Generation Company Limited kinachojihusisha na uchakataji wa taka kilichoko Kisarawe mkoani Pwani.

Mkurugenzi Mkuu wa Bodi hiyo, James Mbalwe alisema mashine zilizoteketezwa ni sehemu ya zilizokamatwa na bodi hiyo kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi kuanzia mwezi Julai hadi Agosti mwaka huu katika mikoa ya Pwani, Lindi, Kilimanjaro, Dar es Salaam, Morogoro, Manyara na Songwe.

Alisema mashine hizo zilikamatwa kwa sababu mbalimbali ikiwamo kufanya biashara bila leseni, kuingizwa nchini kinyemela, kufanya biashara katika maeneo ambayo hayaruhusiwi na kukwepa kodi.

"Kwa ujumla, mashine hizi zinaitia hasara serikali jumla ya Sh. milioni 33 kwa mwezi, sawa na Sh. milioni 400 (kiwango halisi Sh. milioni 396) kwa mwaka pamoja na kukwepa kodi na tozo mbalimbali kinyume cha sheria.

"Kibaya zaidi waendeshaji haramu wamekuwa wakiwaruhusu watoto kushiriki michezo hiyo, kitu ambacho ni kinyume cha sheria," alifafanua.

Vilevile, alisema katika operesheni hiyo, walifanikiwa kuwakamata watuhumiwa wanane na kuwafikisha mbele ya vyombo vya sheria na mashauri yao yako kwenye uchunguzi.

"Mashine tulizozikamata ni 416, lakini leo (juzi) tumeteketeza mashine 300 kwa sababu hizo 116 zipo nje ya mkoa huu. Hizo nazo tutazileta hapa zitateketezwa. Baada ya kuwakamata tumechukua hatua kadhaa lakini baadhi yao wamelipa faini na wengine walikimbia kwa sababu walikuwa wanaendesha biashara hiyo kinyemela.

"Watu wanapaswa kutambua kuwa mashine hizi hazitakiwi kuendeshwa kwenye nyumba ya mtu, hazitakiwi kuendeshwa karibu na shule, hospitali, maeneo ya Usalama wa Taifa, maeneo yanayohusu watoto pamoja na sehemu ngumu kufikiwa na Jeshi la Polisi," alikumbusha masharti ya leseni za michezo hiyo.

Kiongozi huyo pia aliwataka wananchi kufuata sheria huku akionya wanaomiliki wa mashine wenye leseni kuendesha michezo hiyo pasi na kufuata sheria.

"Lakini pia nionye wale wate wanaoingiza mashine hizi kwa njia haramu nchini, sasa hivi tuko macho kila idara, tumejipanga kila kona kuhakikisha hilo halitokei. Nitoe onyo waache mara moja," alisisitiza.

Mkurugenzi Msaidizi wa Kiwanda cha Chilambo Generation Company limited, Benither Gidioni alisema shughuli yao kuu ni kuchakata taka hatarishi na kuzihifadhi ili zisilete madhara katika jamii.

"Sisi ni kampuni, tunajishughulisha na taka hatarishi, tunazivunjavunja, hasa za umeme na kuzihifadhi kama leo (juzi) unaona tumepokea mashine 300 toka Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania. Kwa hiyo, tutazibomoa na baada ya hapo tutapeleka kwenye viwanda vya kuyeyusha taka

"Ombi langu watu wakiwa na taka, wasisite kuleta hapa, ni mahali sahihi kwa kuchakata taka hatarishi, tunahakikisha zinapotoka hapa haziwezi kuleta madhara. Kwa hiyo, taka za umeme na kemikali chafu hapa ndipo mahala pake kama walivyofanya GBT," alitamba.

# RC: Wakulima wa miwa wasajiliwe kupata mbolea

**Na Mwandishi Wetu** MOROGORO

MKUU wa Mkoa wa Morogoro, Fatma Mwasa ameagiza mrajisi kuhakikisha ifikapo Novemba 30 mwaka huu, wakulima wote 9,500 wa miwa wa Bonde la Kilombero wawe wamesajiliwa ili kupata ruzuku ya mbolea.

Amesema serikali imeshatoa ruzuku ya mbolea lakini kikwazo kikubwa ni wakulima kutosajiliwa.

Mwasa aliagiza hayo juzi wakati akiwasilisha salamu za Waziri wa Kilimo, Hussen Bashe katika maonyesho ya Siku ya Wakulima wa Miwa Bonde la Kilombero yaliyofanyika katika Kijiji cha Ruaha wilayani Kilosa mkoani Morogoro.

Maonyesho hayo yaliandaliwa na Kampuni ya Sukari Kilombero kwa kushirikiana na wadau wa tasnia ya sukari ikiwamo Bodi ya Sukari Tanzania (SBT), TARI-Kibaha, Chuo cha Sukari (NSI), Taasisi ya Kimataifa ya Uhifadhi wa Mazingira (UCN) na Taasisi ya African Wildlife Foundation (AWF).

"Kama ilivyo kaulimbiu ya maonyesho haya inayosema 'Kilimo Bora cha Miwa kwa Utoshelevu wa Sukari Tanzania', ninatoa wito kwa wakulima wa miwa kuhakikisha wamesajiliwa ili kutumia fursa ya ruzuku ya mbolea," aliagiza.

Katika hotuba hiyo, Mwasa alihimiza ushirikiano katika kutafuta suluhu ya matatizo mbalimbali na kuboresha tija ikiwamo matumizi ya mbegu bora, upatikanaji wa mitaji kwa wakulima na miundombinu ya usafirishaji.

Mkurugenzi wa Bodi ya Sukari Tanzania, Prof. Kenneth Bengesi alisema maonyesho hayo ni fursa kwa wadau wa tasnia ya sukari kubadilishana ujuzi na kujifunza teknolojia mbalimbali za kilimo cha miwa kama jitihada za kukuza ufanisi wa tasnia katika kuiwezesha nchi kuwa na utoshelevu wa sukari.

Akizungumza katika maonyesho hayo, Prof. Bengesi alisema, "Tunataka kuhakikisha viwanda vilivyopo vinaongeza uwezo wa kuzalisha sukari kwa kufanya mabadiliko kupitia mikakati kama upanuzi wa viwanda, kilimo cha umwagiliaji na ujenzi wa viwanda vipya."

Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni hiyo, Guy Wiliams alisema kuwa kupitia mradi wao wa upanuzi, watasaidia kuongeza idadi ya wakulima wa miwa kutoka wakulima 9,000 hadi takriban 12,000 pamoja na kuzalisha ajira 2,000 katika mnyororo wa thamani.

RIPOTI MAALUM-2

# Wanaume wanavyotelekeza familia kisa ukosefu wa samaki

Na Augusta Njoji aliyekuwa
MTERA

**KATIKA sehemu ya kwanza ya ripoti hii jana, kulikuwa na ufafanuzi kuhusu shida zinazoikabili jamii ya Mtera wilayani Mpwapwa mkoani Dodoma kutokana na kuadimika kwa samaki kwenye Bwawa la Mtera. Endelea kufuatilia kinachowasibu na mustakabali wake.**



Wauzaji wa samaki katika geti la Mtera wakisubiri wateja kwenye barabara ya Iringa-Dodoma eneo la Mtera. Samaki wanaouzwa eneo hilo kwa sasa wanatoka Tabora baada ya Bwawa la Mtera kukumbwa na uhaba wa samaki. **PICHA: AUGUSTA NJOJI**

### WAVUVI WABAKI 10

MWENYEKITI wa Kitongoji cha Chungu, Andrew Kiparamoto, anasema ni mwaka wa nne sasa hali ya bwawa hilo sio nzuri na kuathiri uchumi wa wananchi wake.

"Wengi wamehama na kutelekeza familia na kufunga biashara, kinababa wametelekeza wake zao na watoto,"anasema.

Kiongozi huyo anasema amekuwa akipokea malalamiko kutoka kwa kinamama kuwa hata wakiwapigia simu waume zao kuwajulisha kuhusu hali za familia, nao wanawapa mrejesho kwamba huko waliko nako hali sio njema kiuchumi.

"Wanawake wanasema hata kinachotumwa wakati mwingine hakikidhi mahitaji kwa sababu mtu ameacha mke na watoto, tena wanasoma na wana mahitaji ya shule, chakula lakini anatuma Sh. 10,000, anafika kwa wakala anapata Sh. 8,000 halafu unasema atumie kwa makini baada ya mwezi wakati hata mahitaji ya siku moja haitoshi," analalamika kiongozi huyo.

Anasema wanawake waliotelekezwa na waume zao wanaishi kwenye mazingira magumu.

"Hakuna mzunguko wa fedha, nilikuwa na maduka sita lakini yanayotoa huduma kwa sasa ni mawili, mengine yamefungwa. Hakuna kipato kabisa, nilikuwa na wavuvi zaidi ya 300, sasa hawazidi 10," anabainisha.

Kiparamoto anasema serikali iangalie namna ya kutoa mikopo yenye riba nafuu ili wanawake wafanye ujasiriamali utakaosaidia wajikwamue kiuchumi na kutoa huduma kwa familia zao.

### UONGOZI KIJIJINI

Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Mtera, Angela Minja anasema pamoja na mabadiliko ya tabianchi kuathiri upatikanaji wa samaki kwenye bwawa hilo, pia kuna shida nyingine ya nyavu zinazoitwa 'timba' zilizotumika kwenye uvuvi haramu na kusababisha uhaba huo.

Anasema kwa sasa hali ni mbaya kwenye eneo hilo kutokana na watu kuhama na kibaya zaidi kuna anachokiita kinababa kuacha kinamama na watoto.

"Katika suala la kuacha shule, tumeshaletewa majina ya wanafunzi hapa ofisini ambao walifaulu kuingia kidato cha kwanza, tukaita wazazi ambao wa kike ndio wanapatikana wanasema fedha za kununua sare za shule na madaftari hawana na baba zao hawapatikani, kwamba wanapoondoka hata mawasiliano yanakuwa magumu.

"Hali ya kiuchumi sio nzuri, ninaletewa malalamiko mengi hapa ofisini kinamama uchumi umeyumba, wanalazimika kuingia kwenye mikopo.

"Mama anashindwa kuhimili familia, anaingia kwenye mkopo, mwisho wa siku anashindwa kulipa mikopo na kufunguliwa mashtaka, mpaka sasa malalamiko ya namna hii tumepokea zaidi ya 20.

"Wakiulizwa, wanasema ni hali ya kiuchumi na waume zao wameondoka na hawapatikani, kwamba ameenda kwa shughuli za kiuvuvi Tabora, Singida au Bahi," anafafanua.

Ofisa huyo anasema halmashauri ilikuwa inategemea mapato mengi kwenye shughuli za uvuvi, akibainisha kuwa kata nzima kwa mwezi ilikuwa inapata kati ya Sh. milioni nne na sita lakini kwa sasa hata kwa siku wanaweza wasikusanye mapato yoyote na kwa mwezi mapato ya samaki hata Sh. 100,000 hazifiki.

"Hali imekuwa mbaya wilayani wanakuja wanaangalia hadi bwawani lakini hamna kitu. Kila siku wavuvi wanakuja kuchukua barua za kusafirisha mitumbwi yao kupeleka maeneo mengine, wanasema hali ya hapa ni mbaya.

"Mwenyekiti wetu wa kijiji sisi ni mvuvi, hayupo kwa sasa, kaondoka. Hata wajumbe wa serikali ya kijiji wamebaki 10 kati ya 25 wanaotakiwa. Kuna wakati hata shughuli za kiserikali zinazohitaji uamuzi wao inakuwa tatizo kwa sababu akidi ya vikao haitimii," anasema.

Hoja ya uvuvi haramu kuwa sehemu ya uhaba wa samaki kwenye Bwawa la Mtera, inaungwa mkono na mvuvi Kodi anayesema bwawa hilo lina aina mbalimbali za samaki lakini wanaoongoza na kukuza uchumi kwa haraka ni perege ambao sasa hawapatikani huko.

"Uvuvi haramu umechangia hali hii. Miaka ya nyuma wakati samaki wanatoka kulikuwa na uvuvi haramu uliokithiri, kuna nyavu za sumu aina ya timba zimechangia sana, wataalamu wanasema nyavu hizo hutumika kwa ajili ya utafiti na zinatoka Kigoma, Tunduma na Zambia," anasema Kodi.

### MAHUDHURIO SHULENI

Mwalimu wa Taaluma katika Shule ya Msingi Mtera Dam, Fadhilahi Mkulungu anasema mahudhurio ya watoto yameathirika kutokana na wakazi wengi wa eneo hilo kuwa wavuvi.

"Kuna utoro wa rejareja, yaani kuna kundi ambalo wamehama na watoto lakini kuna ambao wamehama lakini wameacha watoto, unakuta ndio tatizo kubwa. Kuna watoto sasa wamegeuka kuwa wazazi, ni tatizo ambao linatuathiri kwa sasa," anasema.

Anatolea mfano kuwa darasa la saba shuleni kwake mwaka huu likuwa na wanafunzi wasiopungua 15 ambao walikuwa na mahudhurio ya kulegalega na kati yao, sita wameshindwa kufanya mtihani wa kuhitimu elimu ya msingi.

"Kwa darasa la nne pia kuna watoto zaidi ya 15 ambao hadi sasa huenda wasifanye mtihani kabisa kutokana na utoro kutohudhuria shuleni zaidi ya miezi miwili, dakika za mwisho hizi tunawatafuta," anasema.

### KAULI YA DED

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa, Mwanahamisi Ally anafafanua kuwa Bwawa la Mtera linagusa pande tatu za Mpwapwa, Chamwino na Iringa na kila upande una shughuli zake.

"Upande wetu (Mpwapwa) ni eneo dogo ambalo samaki wanazaliwa, kwa asilimia kubwa wanazaliwa upande wa Chamwino, kama kuna shughuli za kibinadamu zinafanyika kule, samaki hawawezi kupatikana hapa kwetu.

"Mfano, kwa Iringa upande wa Magoli, kuna watu wanalima, wanapolima huko wanatumia dawa au mbolea kustawisha mazao yao. Kwa hiyo, athari zitakazopatikana Iringa au Chamwino lazima na kwetu Mpwapwa zitatuathiri, hivyo menejimenti yake inahitaji wilaya zote tatu zikubaliane kama ni kuacha hizo shughuli za kibinadamu.

"Tuliunda timu ilikwenda kufuatilia ikakuta kweli sisi huku tunaathirika kwa sababu samaki wanatakiwa wazaliwe wanakozaliwa halafu huku kwetu wanakuja, mazalia mengi yanaonekana yako upande wa Chamwino, sasa kama kule hawazaliwi, basi kuwapata huku kwetu ni shida.

"Inasemekana pia njia za uvuvi huko nyuma walikuwa wanatumia kemikali na makokoro, hivyo hali hiyo ilisababisha uharibifu mkubwa maana walivuliwa hadi wale wadogo kama dagaa, kama unatumia kemikali kuua kile kizazi ni rahisi, kwa kweli mambo mengi yanazungumzwa kutokana na ukosefu wa samaki.

"Sekta zinazohusika yaani Wizara ya Uvuvi na Wizara ya Kilimo wamekuja na kuangalia lakini kubwa zaidi pale sasa hivi sasa samaki hakuna, ni peupe, hata wavuvi wamehama, kuna jambo kubwa linabidi lifanyike kwa wilaya zote zinazozunguka bwawa tukae tuwe na sauti moja na mkakati mmoja," anashauri.

Mkurugenzi huyo anasema hatua mojawapo anayoona inastahili kuchukuliwa kwa sasa ni kulifunga bwawa na kuzuia shughuli zote za uvuvi na kuleta tena vifaranga vya samaki.

Anakiri kuwapo taarifa za wanaume wavuvi kuhama kwenye maeneo hayo na kwenda sehemu zenye samaki na kuzitelekeza familia zao.

"Tunaposema watu wa Mtera wamepata athari, hakuna samaki, unakuta na kwenye kilimo pia mazao hakuna, ukija kwenye ufugaji nao wana changamoto zao. Sisi tunaangalia wote waliokuja na changamoto wanataka kukopeshwa au kusaidiwa kwa namna Fulani, wote tunawaangalia.

"Bado hatujapata mama aje aseme 'mimi nimeathirika na shughuli za uvuvi kule', kilichopo wanakuja watu kuomba mikopo kufanya shughuli fulani na uwezeshaji wa wanawake kupitia mikopo ya asilimia 10 ya mapato ya halmashauri tunawapatia. Tunajua mwanamke akipata akafanya shughuli zake kupitia uwezeshaji huo, watoto watapata huduma.

"Pia kutoka kwa mikopo inategemea na mapato na pia kulingana na mahitaji. Unaweza kupata watu wengi kila mmoja anahitaji lakini kutokana na fedha zilizopo tunaangalia nani apewe kwa kipindi hiki, kwa wale ambao wapo mazingira magumu, wananufaika kupitia Mfuko wa TASAF.

"Mikopo tunatoa kulingana na kigezo cha mtu aliyeomba na sifa zake zikimbeba, lakini pia kuwapo kwa fedha kama hazitoshelezi huwezi fikia wilaya nzima. Tunafahamu watu wanahitaji ni jukumu letu tunaendelea kupambana hivyo hivyo," anasema.

Mwanahamisi aanabainisha kuwa mapato yanayotokana na uvuvi kwa sasa Mtera hayapo na kwamba kwa mwaka jana hakuna kilichokusanywa katika sekta hiyo.

"Na mwaka huu tunaona dalili ipo vilevile, hadi kamati ya ALAT Mkoa limezungumzwa hilo, watu wakajaribu kujadili sasa inakuwaje? Pale inahitajika kazi kubwa ya kurudisha hali Mtera iwe kama ya mwanzo ya kupishana na samaki Mtera.

"Kwa sasa ukiona Mtera samaki unaambiwa wanatoka Singida au Tabora, kwa kuwa pale wamejulikana ni sehemu ya samaki, kwa hiyo mtu anachukua huko anakuja kuuzia pale, lakini sio samaki wa Mtera," anabainisha.

Kuhusu kudorora kwa mahudhurio ya wanafunzi katika baadhi ya shule, mkurugenzi huyo anakiri kuwapo utoro na wanaendelea kuchukua hatua ili kudhibiti hali hiyo.

## Tanzania ilivyouza tani 3,200 nyama ughaibuni

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KATIKA kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka 2022/23 Tanzania imeuza tani 3,256.6 za nyama nje ya nchi zenye thamani ya dola za Marekani milioni 13 huku lengo likiwa ni kuuza tani 16,000 ifikapo mwaka 2026.

Msajili wa Bodi ya Nyama Tanzania (TMB) Daniel Mushi, alibainisha hayo jana jijini hapa alipotoa taarifa ya utelezaji wa shughuli mbalimbali za bodi hiyo kwa waandishi wa habari.

Alisema moja ya mikakati ya bodi hiyo ni kuongeza kiasi cha nyama kinachouzwa nje ya nchi kwa kushirikiana na viwanda vya nyama na wafanyabiashara wanaouza nyama nje ya nchi.

"Mikakati mingine ni kulinda masoko ya nyama tuliyonayo. Kwa sasa tunauza nyama Qatar, UAE (Umoja wa Falme za Kiarabu), Bahrain, Kuwait, Oman, Comoro, Hong Kong, Jordan na Saudi Arabia.

"Mwaka jana tuliuza tani 10,415 zenye thamani ya dola milioni 42, robo ya kwanza ya mwaka huu wa 2022/23 tumeuza tani 3,256.6 za nyama nje ya nchi zenye thamani ya dola za Marekani milioni 13. Lengo ni kuuza tani 16,000 ifikapo mwaka 2026," alisisitiza.

Alisema mkakati mwingine ni kuhamasisha unenepeshaji wa mifugo ili kupata mifugo iliyo bora ambayo ni malighafi katika viwanda vya nyama ambapo hadi sasa wamewapa mafunzo wanenepeshaji 506.

Pia tunapanga kuhamasisha wafugaji kubadilika kutoka ufugaji wa mazoea na kuanza kufuga kibiashara, kutangaza fursa mbalimbali za uwekezaji zilizoko kwenye mnyororo wa uzalishaji nyama na bidhaa za nyama zikiwamo machinjio, viwanda vya kuchakata nyama, mifumo ya ubaridi na unenepeshaji.

Alisema mkakati mwingine ni kuhamisha uundwaji wa vyama vya wadau ili vifanye shughuli zao kwa ufanisi, kuhamasisha wadau kufuata sheria, kanuni na taratibu za kufanya kazi katika mnyororo wa thamani wa nyama ili zao la nyama linalopatikana liwe bora na salama kwa mlaji.

"Kuhamasisha ulaji nyama unaotakiwa ili Watanzania wawe na afya bora na kinga ya mwili inayoweza kupambana na magonjwa nyemelezi ambapo hadi sasa takwimu zinaonyesha kuwa ulaji wa sasa ni kilo 15 kwa mwaka badala ya kilo 50 kwa mtu mmoja kwa mwaka unaotakiwa," alifafanua.

Vilevile, alisema kutokana na utekelezaji wa kazi zilizopangwa na bodi kama vipaumbele vyake katika mwaka wa 2022/23, wananchi watanufaika kwa njia mbalimbali ikiwamo kuongezeka kwa ubora na usalama wa nyama inayopatikana sokoni na kulinda afya za wananchi kupitia mafunzo yanayotolewa na ukaguzi wa kazi za wadau.

Mushi alisema ukaguzi utakaofanywa na bodi utasaidia wazalishaji wa nyama na bidhaa zake kufikia viwango vya kitaifa na kimataifa.

# WB, serikali washuhudia mikataba ya ujenzi NIT

**Na Mwandishi Wetu**

CHUO cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) kimeingia mikataba ya ujenzi wa majengo matano yatakayojengwa katika kampasi kuu ya Mabibo mkoani Dar es Salaam kwa ufadhili wa mradi wa Benki ya Dunia wa EASTRIP.

Kabla ya kutiwa saini mikataba hiyo ambayo ujenzi utatekelezwa na kampuni ya CRJE (East Africa) Ltd na Nandhra, Mwakilishi wa Benki ya Dunia nchini, Dr. Xiaoyan Liang alisema: "Benki ya Dunia imejiridhisha na mafunzo yanayotolewa katika Chuo cha Taifa Cha Usafirishaji, hivyo tutaendelea kushirikiana nao kwani tumeona mafanikio mbalimbali yakiwamo kwa wahitimu kupata ajira ambapo baada ya utafiti kufanyika zaidi ya asilimia 61 ya wahitimu wamepata ajira.

"Mafanikio hayo ni chachu kwa chuo ambapo tumeona ongezeko la udahili wa wanafunzi kutoka 4,000 mpaka 8,000 kwa sasa."

Alisema chuo hicho ni moja ya vyuo ambavyo vinafadhiliwa na Benki ya Dunia kupitia mrad wa EASTRIP huku Mkuu wa NIT, Prof. Zacharia Mganilwa akisema ujenzi wa majengo hayo matano utakamilika baada ya mwaka mmoja. "Kwa namna ya pekee niwashukuru Benki ya Dunia kwa kufadhili kituo chetu cha umahiri ambacho ni cha muhimu sana kwa ustawi wa sekta ya uchukuzi na sekta ndogo ya usafiri wa anga nchini," alisema.

Aliongeza kuwa NIT ni moja kati ya vyuo vinne nchini vinavyotekeleza mradi huo wa kikanda kwa kuanzisha Kituo cha Umahiri cha Mafunzo ya Taaluma za Usafiri wa Anga na Operesheni za Usafirshaji (CoEATO).

"Kituo hiki cha umahiri ni cha kipekee katika mradi wa EASTRIP na katika nchi yetu ya Tanzania chenye malengo ya kutoa wataalamu wabobezi katika fani za usafiri wa anga ili kupunguza uhaba wa wataalamu katika sekta ya usafiri wa anga na operesheni za usafirishaji hapa Tanzania na Afrika Mashariki," alisema.

Alibainisha kuwa kupitia mradi wa EASTRIP, NIT itapata fedha dola za Marekeni milioni 21.25 sawa na Sh. bilioni 49.053 kwa ajili ya kuimarisha utawala na mafunzo katika Taaluma ya Usafiri wa Anga kupitia CoEATO.

"Malengo ya mradi huu yanakaguliwa na kuhakikiwa na Price Water Coopers (PwC) ambaye ni mkaguzi wa kujitegemea. Na kwa muda wa miaka mitatu ya utekelezaji wa mradi tayari tumeshafikia malengo ya mradi kwa zaidi ya asilimia 75, na hivyo kupata dola milioni 11.372 sawa na Sh. bilioni 26.343 ambazo ni sawa na asilimia 53 ya fedha zote za mradi kwa NIT," alisema.

Mkuu wa Chuo alisisitiza: "Wiki hi, tumekamilisha ukusanyaji wa taarifa kwa ajili ya ukaguzi na uhakiki wa malengo ya mradi kwa mwaka wa nne na tunatarajia kupata zaidi ya Sh. bilioni 15 kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu."

Akizungumza wakati wa hafla hiyo, Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (Elimu), Prof. Carolyne Nombo alisema serikali itasimamia mradi huu kuhakikisha malengo yanafikiwa.

"Kwa makandarasi ninawaomba mfanye kazi kwa bidii na weledi ili kuhakikisha mradi unakamilika kwa muda uliopangwa, yaani miezi 12," aliagiza Prof. Nombo.

Mkuu wa Wilaya ya Ubungo, Kheri James aliipongeza NIT kwa kutengeneza mazingira mazuri ambayo yanatoa wanafunzi wenye weledi wa hali ya juu katika sekta ya usafirishaji na kuahidi kutoa msaada wa hali na mali ili chuo kifanikishe malengo yake.

"Ninafurahi kusikia kuwa chuo kimeanzisha kozi ambazo hata kwa nchi za Afrika ya Mashariki hakuna. Hivyo, tutaendelea kukipa msaada wa kutosha chuo hiki kiweze kufikia malengo," aliahidi.



Mkuu wa Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT), Prof. Zacharia Mganilwa (kushoto) na Naibu Mkurugenzi wa Kampuni ya CRJE (East Africa) Ltd, Zhang Cuishan, wakitiliana saini mikataba ya ujenzi wa majengo ya chuo hicho, jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ndalichako atoa wiki mbili kwa kiwanda kuboresha mazingira

**Na Frank Monyo**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu), Prof. Joyce Ndalichako ametoa wiki mbili kwa uongozi wa Kiwanda cha Tanzania Ruidar Co. Ltd kuboresha mazingira ya kazi ambayo yameonekana kuwa hatarishi kwa afya na usalama wa wafanyakazi.

Alitoa agizo hilo juzi baada ya kufanya ziara katika kiwanda hicho kinachozalisha bidhaa mbalimbali za plastiki zikiwamo mabomba ya maji na vyombo vya majumbani Kigamboni mkoani Dar es Salaam.

Katika ziara hiyo, Waziri Ndalichako alifuatana na Mkuu wa Wilaya ya Kigamboni, Fatma Nyangasa, Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA), Khadija Mwenda na watendaji wengine wa taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

"Mwenye kiwanda asitishe kwanza shughuli hasa kwenye maeneo yale yanayozalisha maji machafu na maeneo mengine ambayo tumekuta yana mpangilio mbaya wa malighafi na vifaa vya kufanyia kazi ili aweke mazingira vizuri.

"Tumekubaliana naye kufanya hivyo na ahakikishe kwamba katika kipindi anachofanya maboresho, wafanyakazi wanashiriki shughuli hiyo na awalipe stahiki zao kama kawaida," aliagiza.

Prof. Ndalichako alisema kuwa pamoja na kwamba serikali inawapenda wawekezaji, inawataka wazingatie sheria za nchi ikiwamo kuweka mazingira ya uzalishaji katika hali nzuri, ili kuwaepusha wafanyakazi na magonjwa na ajali zinazoweza kusababishwa na maeneo ya kazi yasiyokuwa rafiki.

Akizungumza katika ziara hiyo, Nyangasa alitaka maboresho hayo yafanyike kwa kuwatumia wafanyakazi wao na kusimamiwa na watendaji wa ofisi yake pamoja na wale wanaotoka katika taasisi chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

Meneja wa Kiwanda hicho, Zhang Ping aliahidi kufanya maboresho yaliyoelekezwa na wataalamu ndani ya muda uliokubaliwa na pande zote mbili.

Mtendaji Mkuu wa OSHA, Khadija Mwenda aliwataka wenye viwanda kuwajali wafanyakazi ambao ndio msingi mkubwa wa uzalishaji kwa kuwapa vifaa kinga stahiki pamoja na mahitaji mengine muhimu.

Akizungumza mara baada ya ukaguzi kufanyika katika Kampuni ya Lake Oil Group wilayani humo, Mwenda alisema wamebaini baadhi ya wafanyakazi hupatiwa vifaa kinga na wengine hawapewi.

"Wafanyakazi hawapatiwi maji safi na salama ya kunywa kama ilivyoelekezwa na Sheria ya Afya na Usalama Mahali pa Kazi, jambo ambalo ni muhimu sana hususan kwa wafanyakazi wanaofanya kazi kwenye maeneo yenye joto kali," alisema.

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Ni mwafaka sasa serikali kutunga sheria kudhibiti ukatili wa wenza

**KATIKA** miaka ya karibuni kumekuwa kukitolewa taarifa juu ya matukio mbalimbali ya mauaji ya kikatili yakiwamo ya wanandoa ambayo yamesababisha doa kubwa kwa taifa na sababu kubwa zikitajwa kuwa ni wivu wa mapenzi na baadhi ya wenzi kutokuwa waaminifu katika ndoa zao.

Matukio hayo yamekuwa yakiripotiwa mara kwa mara na makamanda wa polisi wa mikoa pamoja na viongozi wa serikali za mitaa na yamechangia kwa kiasi kikubwa kupotea kwa nguvu kazi ndani ya jamii. Sambamba na kupoteza nguvukazi, pia yamesababisha watoto kuishi na mzazi mmoja au kuachwa yatima. Katika baadhi ya matukio hayo, baadhi ya wenza wamekuwa wakiwaua wenzi wao kisha kujiua ama kwa kujinyonga au kutumia silaha. Hatua hiyo inachangia kuwapo kwa athari mbalimbali katika jamii zikiwamo watoto kuishi na mzazi mmoja au kukosa wazazi wote wawili.

Hali hiyo pia husababisha ndugu kubaki na mzigo wa kuwalea na wakati mwingine kushindwa kuwatimizia haki zao kwa sababu ya uwezo mdogo wa kiuchumi. Wakati mwingine mambo hayo yamesababisha ongezeko la vijana wadogo wanaojiingiza katika vitendo vya uhalifu, maarufu kama 'panya road'.

Kutokana na kasi ya vitendo hivyo vya kikatili, viongozi mbalimbali wakiwamo wa serikali na wa dini wamekuwa wakitumia nafasi zao kuwataka wananchi kuacha kujichukulia sheria mikononi kwa kuwaua wenzi wao na badala yake wameshauri kuwapo kwa suluhu baina ya wahusika na ikibidi kutengana badala ya kukatishana uhai jambo ambalo ni makosa mbele za Mwenyezi Mungu.

Kuenea kwa vitendo hivyo kumewaamsha wadau mbalimbali zikiwamo asasi za kiraia kuingilia kati na kutaka wanaokumbwa na vitendo hivyo waripoti katika vyombo husika ama kwa kusuluhishwa au kutoa taarifa ili sheria ichukue mkondo wake.

Aidha, juzi baadhi ya asasi zilikutana jijini Arusha pamoja na mambo mengine, kujadiliana namna ya kutatua tatizo hilo ambalo sasa limekuwa kama donda ndugu ndani ya jamii ya Watanzania. Wadau hao, katika mkutano wao, wamependekeza serikali kuchukua jambo hilo kama la dharura kwa kutunga sheria ya kudhibiti ukatili majumbani ambako ndiko chimbuko kubwa la matukio hayo. Akizungumza katika mkutano huo uliohusisha viongozi wa dini, serikali na waathirika wa matukio hayo, Mkurugenzi wa Sera, Uchechemuzi na Maboresho wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Fulgence Massawe, alisema wameona kuna umuhimu wa kukabiliana na matukio hayo na kushauri serikali namna bora ya kukomesha matukio hayo ambayo kila kukicha yanazalisha walemavu na vifo.


Kwa mujibu wa Massawe, ili kuhakikisha vitendo hivyo vinapungua au kumalizwa kabisa, wameona ni muhimu kuandaa mpango mkakati utakaotoa picha ya kukabili tatizo pamoja na kuishauri serikali kutunga sheria kwa sababu matukio mengi ya mauaji yanawakumba wenza katika nyumba zao.

Katika matukio hayo wanandoa wamekuwa wakikatana mikono, kuumizana maeneo mbalimbali ya miili na baadhi kupata ulemavu wa kudumu. Kama ilivyobainishwa, matukio ya mauaji ya wanandoa yamekithiri na baadhi yao wamedhalilishwa kwa kufanyiwa ukatili wa kingono au kuumizwa.

Moja ya matukio yaliyoshuhudiwa katika mkutano huo ni la unyama aliofanyiwa mwalimu mmoja na mwenzi wake kwa kukatwa na mume wake kiganja cha mkono wa kulia na sime nyumbani kwake. Sababu kubwa ya kufanyiwa hivyo ni wivu wa mapenzi baada ya mume kushindwa kumkuta mke wake nyumbani wakati akiwa amekwenda kununua mahitaji ya nyumbani.

Kama ilivyoshauriwa na wadau hao, ni wakati mwafaka sasa kutungwa kwa sheria itakayosaidia kudhibiti matukio hayo ya kikatili dhidi ya wenza kwa sababu kama hali itaendelea kwa namna ilivyo sasa, kuna uwezekano jamii ikashuhudia ongezeko la hali ya juu la ukatili.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Sabato Kasika

## Muungwana Lazima Nilonge

## Vyuo vya ufundi viwe tegemeo ajira kwa vijana

**SERIKALI** inaendelea kujenga Vyuo vya Ufundi Stadi (VETA) ili kusaidia wananchi, hasa vijana, kupata ujuzi na ufundi wa aina mbalimbali utakaowawezesha kujiajiri na kuajiriwa.

Uamuzi huo wa serikali unaelezwa na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa kuwa ni kufungua milango ya ajira kwa kuwa mafunzo yanayotolewa yatawawezesha wahusika kuajiriwa katika sekta mbalimbali ikiwamo ya viwanda.

Kutokana na uamuzi huo, kuna haja kwa vijana kuchangamkia fursa hiyo ya kupata elimu ya ufundi ili iweze kuwasaidia kuchangamkia fursa mbalimbali za ajira, ili kukabiliana na vikwazo vya maisha.

Ikumbukwe kuwa serikali ilishatoa maelekezo kwa halmashauri zote nchini, kuwatambua vijana waliopata ujuzi kwenye vyuo vya ufundi stadi ili kupatiwa mikopo ya vifaa vya fani walizozisomea.

Kwa njia hiyo ni wazi kwamba vijana wanaweza kuondokana na mtindo wa kuzunguka huku na kule kutafuta ajira katika ofisi za umma na binafsi, badala yake wataweza kujiajiri na kisha wao kuajiri wenzao.

Mfano, kijana anaweza kusomea ufundi seremala, ujenzi wa nyumba akajiajiri na hata kufikia kuajiri wengine, hivyo kupunguza tatizo la ajira ambalo kwa ujumla wake ni janga la kitaifa.

Hivyo, kasi ya ujenzi wa vyuo vya ufundi katika maeneo mbalimbali nchini, ingeongezeka zaidi, ili vijana waliohitimu elimu msingi, sekondari na wengine waweze kupata ujuzi utakaowawezesha kuendesha maisha yao.

Kuwa na vyuo vikuu vingi si vibaya, ninadhani vya ufundi vingekuwa vingi zaidi, kutokana na ukweli kwamba si rahisi msomi wa chuo kikuu kuvaa nguo chafu na kujenga nyumba ama kuwa fundi seremala.

Kazi hizo zinafanywa na watu wa kawaida wenye ufundi kutoka vyuo vya ufundi, na ninadhani kwamba vijana waliohitimu elimu ya msingi na sekondari ambao hawana ujuzi wowote ni wengi.

> **Njia mojawapo ya kuwakomboa ni kuwajengea vyuo vya ufundi vingi zaidi na kuweka ada ya kawaida ambayo wataweza kuimudu, ili wapate ujuzi waondokane na mtindo wa kushinda vijiweni bila ujuzi wowote.**

Njia mojawapo ya kuwakomboa ni kuwajengea vyuo vya ufundi vingi zaidi na kuweka ada ya kawaida ambayo wataweza kuimudu, ili wapate ujuzi waondokane na mtindo wa kushinda vijiweni bila ujuzi wowote.

Vyuo vinavyojengwa vinaweza kutoa mafunzo kulingana na mahitaji ya eneo husika na kutumia raslimali zinazopatikana katika eneo ambako chuo kipo, kwani hatua hiyo inaweza kusaidia kuinua maeneo yao wanayoishi.

Lakini pamoja na kwamba halmashauri zimewahi kuelekezwa kuitoa mikopo kwa vijana wenye ujuzi waliosoma vyuo vya ufundi, si vibaya hata vyuo vyenyewe vikawapa wahitimu zana na vifaa vya kazi za kujitegemea.

Wakipewa zana na vifaa mara wanapohitimu mafunzo, vitawasaidia kujiajiri, katika shughuli mbalimbali zikiwamo za ufundi stadi na mafundi mchundo ili kuongeza thamani kwenye uchumi wa nchi.

Pamoja na hayo, ninaamini, vijana wengi wamekuwa wakihitimu vyuo vikuu, na kuzunguka na vyeti vya shule kwa muda mrefu kutafuta ajira, lakini yote hayo ni kwa sababu ya kukosekana kwa matayarisho wakiwa shule.

Ni vyema wakatambua kuwa mambo ya msingi ambayo wanatakiwa kuzingatia wanapojiajiri au kuajiriwa, ni muhimu wawe wamebobea katika fani kadhaa ikiwamo ufundi seremala, uashi, makenika, upishi na mwingine.

Si siri kwamba ukosefu wa ajira umechangia mwelekeo wa baadhi ya vijana na kusababisha kupata vijana wasio waadilifu, waliokata tamaa na kuonekana kama mzigo kwa jamii na kwa familia.

Umefika wakati wa kutochagua ajira kulingana na kile walichosomea vyuo vikuu, badala yake wapate ufundi ili kupata ujuzi na kuchangamkia fursa zilipo hata kwenye maeneo wanayoishi.

SAFU

## FIKRA MBADALA

# Tanzania tuchangamkie fursa za kuwa na majirani wahitaji



Pascal Mayalla

KUNA msemo wa Kiswahili usemao, unaweza kuchagua marafiki lakini huwezi kuchagua majirani. Ili uishi vizuri na majirani zako, unashauriwa ujifunze kuishi nao vivyo walivyo lakini mimi naongezea, ili uneemeke na majirani zako, jifunze kuyajua mahitaji yao ili kama unayo na unaweza kuwasaidia, wasaidie si tu watakushukuru kwa msaada wako, bali utabarikiwa kwa kuwasaidia. Kitu kikubwa zaidi ni wewe utaneemeka zaidi na wewe na jirani zako wote watafaidika.

Tanzania imezungukwa na nchi nane ambazo ni majirani zetu. Nchi hizo ni Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Zambia, Malawi na Msumbiji. Majirani zetu hawa hawafanani, wengine ni wakubwa na wanazalisha karibu kila kitu lakini wengine ni wadogo, wananunua karibu kila kitu.

Katika Jumuiya ya Afrika ya Mashariki (EAC) yenye nchi saba, Tanzania, Kenya, Uganda, Sudan Kusini, Rwanda, Burundi na DRC, Tanzania imepakana na nchi 6 kati ya hizo na zile tatu zilizopakana ni Zambia, Malawi na Msumbiji.

Tanzania inakutana nazo kwenye Jumuiya ya maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC). Kwa mantiki hiyo, Tanzania ndiyo nchi inayoongoza kwa fursa za kufaidika na majirani kwa kuwa mwanachama wa EAC na SADC.

Fursa ni kitu cha kuchangamkiwa. Ikitokea fursa fulani mbele yako, wewe mtu wa karibu usipoichangamkia, jirani yako wa mbali atakupita na atakupiga bao na kukuacha unang'aa ng'aa macho huku fursa zinakupita.

Ukiangalia ukaribu wa baadhi ya hawa majirani zetu na makao makuu ya nchi zao, utakuta kuna maeneo Tanzania ni karibu kuliko makao makuu yao yenye viwanda vya bidhaa.

Wenzetu Wachina, wamepata maendeleo kwa haraka, kutokana na kuzalisha bidhaa ndogo ndogo zinazohitajika, kupitia viwanda vidogo vidogo, kizungu wanaziita 'backyard industries'. Karibu kila nyumba kule nchini China ni kiwanda cha bidhaa ndogo ndogo zinazohitajika kwa matumizi mbalimbali ya wateja.

Ni aibu sisi Tanzania, tunayo miti ya kutosha ya kuzalisha vijiti vya meno lakini makontena ya bidhaa hizo yanayoka China! Wanatuletea 'toothpick' Tanzania na wao kurejea na magogo China kuzalisha zingine na kutuletea.

Hata pini tuu au sindano Tanzania tunaagiza kutoka nje!. Hata vyuzi na nguo pia tunaagiza. Tanzania tunazalisha pamba, tunauza nje, wanatutengenezea nguo, tunaletewa na kuzinunua! Kwa vile umasikini ni mkubwa, Watanzania wenye uwezo wa kuvaa nguo mpya wanahesabika, waliobaki ni kupishana kwenye sagula sagula ya nguo za mitumba! Lakini pia naomba kukiri, baadhi ya hizi nguo za mitumba kutoka Ulaya, zina ubora mkubwa kuliko nguo mpya za kutoka China.

Kama vijijini vyote vya mipakani, vitakuwa na viwanda vidogo vidogo vya kuzalisha bidhaa za walaji, Watanzania tungewapelekea majirani zetu wote bidhaa za matumizi ya kila siku kwa kupatikana karibu zaidi kuliko kuzipata nchini mwao.

Hivi karibuni, nilitembelea jijini Bujumbura nchini Burundi, nikakuta kumbe na wao wameamua kujenga makao makuu yake katika mji mwingine, kama sisi Tanzania tulivyoamua kuhamia Dodoma.

Kwa maana hiyo, Burundi kuna uhitaji mkubwa sana wa vifaa vya ujenzi na hasa saruji. Burundi hawana saruji ya kutosha, hivyo inawabidi waagize kutoka nje.

Baadhi ya sementi wanaagiza kutoka Tanzania lakini haitoshi, hivyo inawabidi kuagiza nyingi zaidi kutoka nchini Zambia ambako ni mbali zaidi na hiyo malighafi ya sementi ya Zambia, inapelekwa kupitia bandari ya Dar es Salaam, kisha inapakiwa kwenye treni ya Tazara ndipo inakwenda Zambia, wanatengeneza sementi, wanamletea jirani yetu wa karibu yetu.

Balozi wa Tanzania nchini Burundi, Dk. Jilly Maleko, ametoa wito kwa Watanzania kuchangamkia fursa mbalimbali za kibiashara kati ya Tanzania na Burundi. Hiki anachofanya Balozi kinapaswa kufanywa na mabalozi wetu wote wa nchi tulizopakana nazo, kuzimulikia fursa za kibiashara za mahitaji muhimu ya nchi walizomo kwa kufanya iteligensia ya kiuchumi kujua nchi hizo zinaagiza sana bidhaa gani kutoka nje.

Baada ya kufanya intelejensia hiyo na kuzijua, taarifa hiyo inaletwa nchini kwa wakuu wa mikoa ya mipakani, serikali iwezeshe kujengwa kwa viwanda vidogo vidogo vijiji vya mipakani, hivyo kuwapatia mahitaji ya kila siku.

Tanzania baada ya kutumia diplomasia ya uchumi, licha sasa duniani hakuna tena vita baridi, lakini kwenye balozi zetu zote bado zina waambata wa kijeshi, nilitegemea baada ya kubadili diplomasia yetu kuwa ni diplomasia ya uchumi, balozi zetu zote ziwe na waambata wa kiuchumi ambao watafanya itelijensia ya uchumi kuwa majirani zetu wanahitaji nini ili tuwapelekee.

Mfano mzuri ni karibu nchi zilizotuzunguka, zinapitishia mizigo yao mingi bandari ya Dar es Salaam na moja ya bidhaa kuu ni magari yaliyotumika. Tanzania tulipaswa siku nyingi tuanzishe bandari hizo ili kampuni kubwa za uuzaji wa magari ziweke yadi zao Dar es Salaam kama ilivyo kwa Dubai.

Kwa kufanya hivyo, nchi zote za Kusini mwa Jangwa la Sahara zisingekuwa na sababu ya kuagiza magari kutoka Japan au Dubai kwa kuwa yadi za Japan na Dubai zitakuwa Dar es Salaam.

Kwa maana hiyo nchi jirani zingekuja Dar es Salaam au kuagiza magari kutokea hapa. Kwa mfumo huo tungefanya biashara kubwa ambayo itaziba pengo la ushuru uliopotea kwa kuanzisha bandari huru.

Tanzania Mungu ametujalia nchi nzuri ya fursa kibao, majirani kibao, wenye mahitaji kibao na fursa kibao za kutimiza mahitaji yao.

Kitu kilichobakia kwa Tanzania ni kuchangamkia fursa za ujirani mwema. Tukitimiza hayo, tutabarikiwa, nchi itabarikiwa, na majirani watatushukuru sana.

***Wasalaam.***
***Paskali***
***+255 754 270403***

## MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Watanzania tunakimbia au tunatambaa?



Na Joseph Kulangwa (kulangwasos@gmail.com)

UKIWA mtu unayefikiria vema, ukikaa na kutuliza akili, utajikuta unaiona Tanzania ikiwa katika sehemu mbili za maendeleo kiuchumi, kijamii na kisiasa.

Mimi mathalan, nikitulia huwa naiona Tanzania kama nchi inayoendelea kwa kasi sana lakini upande mwingine naiona kama nchi inayozaliwa leo au jana na inatambaa.

Ukiitazama miji ya nchi hii utaona jinsi inavyojengwa kwa haraka, utaitazama Dar es Salaam mathalan ina madaraja ya juu katika kila makutano ya barabara zake.

Ukikimbilia Mwanza utakutana na daraja refu linajengwa huku likitishia kuwa refu kuliko yote Afrika Mashariki, na limeshaitwa Daraja la Magufuli.

Lakini haitoshi, ukienda mkoani Pwani utakutana na ujenzi wa daraja la Wami ambalo bila shaka liko ukingoni kabisa na litaanza kutumika saa yoyote, pale Kimara mpaka Kibaha mnajionea wenyewe ile barabara.

Achana na hayo, tunashuhudia miradi ya kimkakati; kuna reli ya kisasa ambayo hata Waziri Mkuu Majaliwa Kassim ameshakwenda Korea Kusini kukagua mabehewa ya treni mpya.

Pale Dodoma ndo usiseme kabisa, Chamwino Ikulu inayofanana na ya Magogoni bila shaka nayo iko ukingoni kukamilika, achana na majengo mengine na miundombninu mingi inayojengwa makao makuu. Bado masoko na stendi za kisasa kila mkoa takribani.

Bwawa la Umeme la Mwalimu Nyerere nalo liko mwendokasi ile mbaya, baada ya muda tutashuhudia umeme wa kumwaga na kuuza nje. Mungu aipe nini Tanzania, inasonga mbele kimaendeleo utafikiri Taifa kubwa kama hayo tunayosimuliwa ya kina Biden, Sunak na Putin.

Lakini upande huu mwingine, nashindwa kuelewa kabisa ni kama nchi inatambaa hivi. Unasikia ziara za viongozi mikoani na wilayani kuhimiza maendeleo, lakini mwishowe wanarudi kukaa na kujipanga upya ili kurudia ziara.

Hebu tazama siku za karibuni, tukasikia kiongozi anapanda helikopta kwenda kukagua vibao vya barabara, yaani vibao vyenye majina ya barabara mikoani na kurudi.

Nendeni mkatazame kama vibao hivyo vimeenea kote. Jijini Dar es Salaam tu ambako mambo mengi huanzia kuna mitaa bado haina vibao ingawa ina majina, sijui kinasubiriwa ziara nyingine ya helikopta!

Kiongozi mwingine unamsikia yuko mikoani anafurumishana na wananchi kuhusu migogoro ya ardhi, lakini utaratibu wa kurasimisha makazi kwa wananchi ulioanza mwaka 2018 ili wapate hati na kuzitumia kukopa na kujiendeleza kiuchumi umekwama.

Wananchi wakiuliza wenye dhamana kwa nini mradi huo ni kama umesimama, majibu ni kwamba baadhi ya wakazi hawajalipa gharama za kazi hiyo, ama kwa kukosa fedha au kwa makusudi tu.

Unajiuliza kwani hati ya nyumba ni ya mmiliki wa nyumba au ni ya kijiji au mtaa? Kwa nini aliyelipia asihudumiwe mpaka kupata hati na badala yake udhaifu au uzembe wa mwingine aambukizwe asiyehusika?

Haitoshi, hivi sasa tunasikia kuna mgawo wa maji! Nchi yenye umri wa miaka 60 leo bado tunazungumzia mgawo wa maji, eti hatuna jinsi ya kupata maji ila kwa mgawo! Yaani tangu nchi izaliwe maji yamekuwa na mawaziri.

Ina maana hakuna waziri kati yao aliyewahi kuja na ubunifu wa kubashiri kwamba miaka fulani ijayo nchi itakuwa na matatizo haya ya maji na hivyo tujipange? Au na hili linatokana na vita vya Urusi na Ukraine?

Tunasikia hivi sasa kuna kampeni kali ya kuhakikisha kina mama zetu vijijini wanatumia gesi kupika badala ya kuni na mkaa, wakitishwa kuwa wakiendelea kutumia nishati hiyo ya asili watakufa kimyakimya!

Hivi kweli kina mama zetu hao watakuja kuwa na uwezo wa kununua mitungi ya gesi na kuhakikisha hawasenyi kuni na kuchoma mkaa? Nchi hii inahitaji uhalisia na ukweli wa mambo, kwani mengine ni nadharia.

Juzi kati hapa lilizuka la tozo kwenye miamala ya simu na kila mmoja aliona kasheshe lake, mpaka Serikali sikivu ikaingilia kati na kupunguza tozo hizo na hiyo ikitokana na kadhia ya utumapo pesa kwa mama kijijini unakatwa, na mama akipokea anakatwa pia.

Kama hilo lilileta kilio iweje sasa tunasisitiza kutumia gesi vijijini? Labda tuambiwe kuwa kutakuwa na mgawo bure wa mitungi ya gesi kila nishati hiyo itakapokuwa ikimalizika, vinginevyo tusidanganyane, tutaendelea kutambaa kama Taifa. Uhalisia utusaidie kidogo basi.

***Alamsiki!***

## Balozi wa Sweden ataka wanawake wawezeshwe

**Na Thobias Mwanakatwe,** IKUNGI

BALOZI wa Sweden nchini, Charlotta Macias amesema nchi zikijenga usawa wa kijinsia na kumwezesha mwanamke kiuchumi, zitaleta mbadiliko ya uchumi, fikra na maendeleo katika jamii.

Alisema hayo juzi wakati akizungumza na wananchi wa Kijiji cha Mnang'ana, Kata ya Sepuka wilayani Ikungi mkoani Singida baada ya kutembelea mradi wa kituo cha huduma kwa wakulima Mnang'ana Amcos.

Katika ziara hiyo, Balozi Macias alitembelea ghala la kuhifadhia mazao lililojengwa na Shirika la Farm Africa kwa ushirikiano wa Shirika la Umoja wa Mataifa linalohusika na masuala ya wanawake UN-Women chini ya ufadhili wa Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Korea (KOICA).

Alisema usawa wa kijinsia ni watu kuwa na haki na uwakilishi wa wanawake na kupata nyenzo za kiuchumi na kufanya mambo kwa kushirikiana kati ya wanawake na wanaume kwa kuwa kufanya hivyo kutasaidia kusonga mbele kimaendeleo.

"Moja kujumlisha moja ni tatu, yaani ninamaanisha unapomchukua mwanamke na mwanaume matokeo yake ni zaidi ya mbili, ni tatu, na tangu nimekuja Tanzania miezi mitatu sasa nimekutana na kinamama imara na wanaume imara sana," alisema.

Meneja Mwandamizi kutoka Shirika la Farm Africa, Tumaini Elibariki alisema mradi unaotekelezwa katika Kijiji cha Mnang'ana unalenga kusaidia wananchi kiuchumi ambao hadi sasa umewafikia zaidi ya wanawake 500 wa kijiji hicho.

Alisema wanufaika wa mradi huo wamepewa mafunzo mbalimbali ya kilimo cha alizeti, kuongeza thamani ya mazao na jinsi ya kutafuta masoko ya ndani na nje ya nchi.

Elibariki alisema wanawake pia wamefundishwa uzalishaji wa mbegu bora, hivyo ni wakati sasa kuongeza kasi ya kilimo kwa kupanua maeneo ya kilimo ili kuwawezesha kuvuna mazao mengi na kupata kipato na soko kubwa.

Mkuu wa Idara ya Kilimo Wilaya ya Ikungi, Gurisha Msemo alisema mradi huo ambao unajulikana kama 'Tuifikie usawa kijinsia wa kumwezesha mwanamke, unatekelezwa katika vijiji vya Kipumbuiko, Irisia, Munyu na Mnang'ana.

Alisema miradi inayotekelezwa ni pamoja na kilimo cha alizeti na mboga za majani, mpango bora wa matumizi ya ardhi na umilikishwaji na mradi wa kupunguza ukatili wa kijinsia.

Msemo alisema katika kuhakikisha miradi hiyo inakuwa na mafanikio, kumejengwa soko la kisasa la mboga mjini Ikungi, kimejengwa kituo cha kutoa taarifa kwa waathirika wa ukatili wa kijinsia na wananchi walionufaika ni kati ya 6,000 na 14,000.

Diwani wa Sepuka, Halima Ng'imba alisema miradi hiyo imesaidia kupunguza migogoro kati ya kijiji na kijiji na pia imetoa uhakika wa maisha kwa wananchi kutokana na kujishughulisha na kilimo.

Miradi hiyo ilianza kutekelezwa wilayani Ikungi Oktoba 2020 ambapo ufadhili wa KOICA utafikia ukomo mwezi Machi mwakani.

# ACT: Tanzania haipaswi kulalamikia uhaba wa maji

**Na Pilly Kigome**

CHAMA cha ACT Wazalendo kimesema Tanzania haipaswi kulalamikia ukosefu maji kwa madai ya kuwepo mabadiliko ya tabianchi kwa kuwa kuna vyanzo vingi vya maji ambavyo havijatumika ipasavyo.

Kauli hiyo ilitolewa jana mkoani Dar es Salaam na Ester Thomas, Msemaji wa Sekta ya Maji na Mazingira wa ACT Wazalendo alipozungumza na waandishi wa habari. Alisema mahitaji ya maji kwa umma yanaongezeka kwa asilimia saba kila mwaka huku uzalishaji wake ukiwa unaongezeka kwa asilimia mbili kwa mwakam akidai sababu kubwa ya uzalishaji kuwa chini tofauti na uhitaji, ni uwezo mdogo wa Wizara ya Maji kusimamia miradi mbalimbali ya maji, jambo linalochangia miradi mingi ya maji kutotoa maji kabisa ama kuzalisha kiwango kidogo cha maji.

Alibainisha kuwa mwaka wa fedha wa 2020/21, uzalishaji wa maji nchini ulikuwa wa asilimia 56 tu ya uhitaji wa maji kwa wananchi, hivyo kusababisha wananchi kutumia muda mwingi na gharama kubwa kutafuta maji.

"Tatizo la maji nchini sio janga la asili, ni uzembe wa serikali kumaliza changamoto hizi kwa kuwa miongoni mwa sababu kuu inayochangia hali hii ni kushindwa kukamilika kwa miradi iliyokaa kwa muda mrefu na mingine kushindwa kutekelezwa," alisema Ester.

Alitolea mfano mradi wa Same-Mwanga-Korogwe wenye uwezo wa kuzalisha maji lita milioni 103.7 na wenye kipande cha tatu cha kusambaza maji katika Mji wa Mwanga kinachogharimu dola za Marekani milioni 36.7 na kipande kingine cha nne kinachohusisha ujenzi wa miundombinu ya kusambaza maji katika Mji wa Same kinachotekelezwa kwa thamani ya dola za Marekani 35.25, kwamba utekelezaji wake ulianza mwaka 2014, yaani miaka minane iliyopita lakini hadi sasa haujakamilika. Alitaja sababu nyingine inayochangia ukosefu wa maji kwa wananchi kuwa ni ubadhirifu mkubwa katika miradi ya maji unaolitafuna taifa. "Kumekuwa na wimbi kubwa la ubadhirifu wa fedha za miradi ya maji inayopelekea ucheleweshwaji wa upatikanaji wa maji katika maeneo husika. Hili linathibitishwa na ripoti ya Mkaguzi wa Hesabu za Serikali (CAG) ya mwaka 2020/21 inayoeleza kuwa kumekuwa na ubadhirifu wa Sh. bilioni 37.1 na dola za Marekani milioni 6.05 ambazo zingewezesha maji kupatikana sehemu husika," alisema.

Akizungumzia bajeti inayotengwa kwa ajili ya maji, Ester alisema eneo hilo linatengewa bajeti finyu licha ya kuwa linahitaji fedha nyingi kwa ajili ya uwekezaji wa miradi ya maji

Alisema katika mwaka huu wa fedha, Bunge limeidhinisha jumla ya Sh. bilioni 709. 361 kwa ajili ya Wizara ya Maji. Kati ya fedha hizo, za miradi ya maendeleo ni Sh. bilioni 657.889 na fedha za matumizi ya kawaida ni Sh. bilioni 57.462.

Alifafanua kuwa ikilinganisha na bajeti ya mwaka uliopita (2021/22), bajeti ya mwaka huu ni pungufu kwa Sh. bilioni 110.381 sawa na asilimia 13.46, akisisitiza kuwa bajeti hiyo ya maji haiendani na mahitaji halisi ya maji nchini.

Alisema chama chao kinarudia mapendekezo yake ya kwenye ilani yao ya 2020-2025 na kuitaka serikali ichukue mkopo nafuu wa muda mrefu wa Sh. trilioni 10 kutoka Benki za Maendeleo ya Afrika ili kutekeleza miradi mikubwa ya maji na deni hilo lilipwe kwa tozo za mafuta.

Alitaja pendekezo la pili ni serikali itoe ruzuku kwa mamlaka za maji ili kuziwezesha kupanua na kuboresha miundombinu ya maji katika maeneo yao.

Pendekezo lao la tatu ni serikali kudhibiti huduma za maji zinazotolewa na watu binafsi ili kudhibiti usalama wa maji na gharama za huduma hiyo.

"Serikali iimarishe Mfuko wa Taifa wa Maji kwa kuupa chanzo cha uhakika cha mapato kutoka ushuru maalum utakaotokana na matumizi ya mafuta ya petroli nchini." aliwasilisha.



Waziri wa Maliasili na Utalii, Balozi Dk. Pindi Chana (wa pili kushoto), akikabidhi vitendea kazi kwa Kamshna Mkuu wa Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), Prof. Dosantos Silayo, baada ya kuzindua Bodi ya Ushauri ya Wizara kwa wakala huo, jijini Arusha jana. **PICHA: ASRAJI MVUNGI**

# Tax: Mfumo wa fedha kwenda SADC kuinufaisha Tanzania

**Na Halfani Chusi**

WAZIRI wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Dk. Stergomena Tax, amesema uzinduzi wa mfumo wa kutuma fedha nje ya nchi uliofanywa na kampuni ya Vodacom, utaongeza pato la taifa na kuvutia wawekezaji.

Akizungumza juzi jijini Dar es Salaam wakati wa uzinduzi wa huduma mpya ya nyongeza ya M-Pesa itakayowezesha kufanya miamala ya kifedha kwenda katika nchi nyingi Afrika, Dk. Tax alisema ni hatua kubwa kimaendeleo.

Alisema mfumo huo ni muhimu kwa wakati huu wa uchumi kidijitali na kwamba kupitia huduma hiyo uchumi wa Tanzania utapaa na kuiletea nchi manufaa makubwa.

"Mwanzoni tulikuwa tunaweza kufanya miamala kwa nchi za Afrika Mashariki tu, lakini sasa Vodacom wametanua wigo mpaka kuzifikia nchi zilizopo katika Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), sekta ya fedha ni muhimu kwenye ukuaji wa uchumi," alisema waziri huyo aliyewahi kuwa Katibu Mkuu wa SADC.

"Serikali tunaona hili ni jambo kubwa sana uchumi wa kidijitali unafanyika kidijitali, kwa hiyo na sekta yako ya fedha lazima iwe katika mfumo huo, hivyo niwaombe Watanzania waliopo ndani na nje ya nchi kutumia mtandao huu kwa sababu utaleta manufaa makubwa kwa nchi yetu," alisema.

Alisema moja ya mpango aliokuwa nao wakati alipokuwa akifanya kazi SADC alikodumu kwa miaka minane, ni kuhakikisha kunakuwapo urahisi wa miamala ya kifedha kati ya Tanzania na nchi zingine.

"Nimefurahi na Vodacom wametimiza ndoto zangu japo mimi siko huko kwa sasa lakini wazo langu limezaa matunda kupitia huu mtandao. Kwa mfano kwa sasa kama mtu yuko Botswana au Afrika Kusini, akikutumia fedha, inafika mara moja tofauti na awali," alisema.

Mkurugenzi wa M-Pesa, Epimack Mbeteni alisema huduma hiyo itafaidisha nchi nyingi za Afrika zikiwamo Zambia, Uganda, Malawi, Rwanda, Afrika Kusini, Madagascar, Msumbiji, Jamhuri ya Kidemkrasia ya Kongo na Sudan Kusini.

"Sasa tumetanua wigo na kuzifikia nchi zote zilizopo ukanda wa SADC na nchi zingine zote zilizopo katika ukanda huo. Tunaona huduma hizi zimekuwa zikiturahisishia maisha kwa wafanyabiashara kwa sababu zamani huduma hiyo ilikuwa inasumbua," alisema.

# MAISHA

OKTOBA 30, 2022

Nipashe

Baba, Mama na Mwana

Jumapili




Ukurasa 13

## Polo za wanaume wembamba



Ukurasa 15

## MAISHA NI NYUMBA

Sababu nyumba kuvuja muda mfupi baada ya kujengwa



Ukurasa 12

## HARUSI




# Uso bila sunzua

Ukurasa 14


# WATOTO

## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA







| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | J | A | Z | W | A |
| | A | | | A | |
| A | M | A | | K | |
| | B | | D | A | U |
| | I | | | T | |
| T | A | M | B | I | |




## TOA TOFAUTI 5




## FUMBO TOTO



Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyopo wazi:
BEI, UMA, WANGA, DUNDA, DEREVA, DUMAZA

## PAKA RANGI




## CHEKA



Alichokifanya daktari

MTOTO Musa alikuwa akizungumza na mama yake, katika maongezi yao alianza kumuuliza kuhusu maua na nyuki.

**Musa:** Eti mama, kwenye maua hapakosi nyuki?

**Mama:** Ndio mwanangu.

**Musa:** Kwa hiyo kila panapokuwa na maua nyuki hujenga mzinga wake?

**Mama:** hapana mwanangu, mzinga wakati mwingine huwa mbali na maua.

**Musa:** Mbona mwalimu alituambia kwenye maua mengi hapakosi mzinga wa nyuki?

**Mama:** Huo ni msemo tu, ukimaanisha kila palipo na neema watu hufika kwa wingi.

**SWALI**

Ziwa Tanganyika linapatikana mikoa gani?

## MAISHA NDIVYO YALIVYO

Na Flora Wingia



# Binti daktari aishia kula jalalani sababu alimdharau mama yake!

***KARIBU tena msomaji wangu tumalizie ile simulizi yetu, kisa cha kweli kuhusu dada aliyemdharau mama yake baada ya kumlea na kumsomesha hadi kuwa daktari. Mafanikio yote yalimfanya asahau hata kufikia hatua ya kumfukuza mama yake pale alipomtembelea mjini alikokuwa akiishi.***

Kwa wasomaji wapya wa kisa hiki, mama alipambana na kumlea binti huyu baada ya kufiwa na mumewe akiwa na umri wa miaka 22 na hakutaka tena kuolewa akaamua kumlea mwanawe. Alipomaliza darasa la saba alifaulu shida ikawa ada.

Bahati nzuri zikatangazwa nafasi za wafadhili kusomesha wenye uwezo mdogo, binti akabahatika kuwa miongoni. Sekondari alifaulu hadi chuo kikuu na kupata kazi ya udaktari.

Lakini ilipita takriban miaka 14 toka aondoke kijijini hakuwahi tena kurudi angalau kumjulia hali mama yake. Kazini na hata kwa marafiki zake akawa anawaambia kuwa hana baba wala mama wala ndugu.

Siku moja akakutana na kijana mmoja wa kijijini kwao, wakasabahiana. Ilikuwa furaha kwa wote. Bibie akamwonyesha hadi nyumbani na kwamba yeye ni daktari mkubwa.

Miaka miwili baadaye, yule kijana alipokwenda kijijini kusalimia jamaa zake, akakutana na mama mzazi wa yule binti daktari, wakasalimiana. Kijana akamwambia mama kwamba alikutana na binti yake na kwamba ni daktari mkubwa.

Mama akashangaa. Akamsihi siku anarudi mjini waende wote ili akamwone kwa macho bintiye. Siku ikawadia wakaondoka wote wakafika nyumbani kwa daktari. Alikuwa bado hajarudi kazini, hivyo mama alimsubiri pale getini walipo walinzi. Kijana akaondoka zake.

Daktari kurejea nyumbani walinzi wakamjulisha kuna mgeni anamsubiri. Mama kumwona akawa anamsogelea amkumbatie kwa furaha ya kutokuonana baada ya miaka mingi. Cha ajabu binti akawa anamwambia usinisogelee wala kunigusa!

Mama hakumwelewa, binti akaingia zake ndani na kumwacha mama getini na walinzi. Baada ya muda mama akaaga walinzi akaondoka. Jirani na nyumba ya mwanawe akaona kanisa, akaingia na kumwomba Mungu amrehemu na amsaidie kwa yaliyotokea.

Mchungaji wa kanisa lile akamfuata mama naye akamweleza kisa chote. Ni usiku tayari, mama akamwambia mtumishi huku anaondoka zake. Ingawa alimsihi sana lakini mama hakukubali, akamuaga na kuondoka! Muda mfupi baadaye, zikasikika taarifa za ajali umbali mfupi toka pale kanisani kuwa yupo mama amegongwa na gari.

Mpenzi msomaji, sasa tuendelee na sehemu ya mwisho ya kisa hiki, ujue hatma ya mama na binti yake ilivyokuwa. Mara baada ya Mchungaji kusikia taarifa za ajali, haraka alifuatilia na kumbe, ni yule mama aliyekuwa akiongoea naye muda mchache uliopita pale kanisani!

Akachukua gari lake kumpeleka hospitalini. Madaktari walipomwona wakagundua alipoteza damu nyingi, hivyo ameshapoteza maisha. Mchungaji alilia sana!

Akampigia simu dada daktari kwani walifahamiana na ni majirani. Akamjulisha kuwa mama yake amefariki dunia kwa ajali. Kusikia vile akahamaki akawa anasema, mama, mama huku akionekana kama anatembea.

Yaani alikuwa akitaja tu neno mama, mama hadi mchungaji akakata simu. Mwili wa mama ukahifadhiwa, akaenda mchungaji nyumbani kwa daktari akaambiwa alivyotoka hajarudi. Hata alipokwenda kazini kwake akaambiwa alitoka akiongea na simu huku akitaja neno mama, mama, hatujui ana shida gani.

Ilikuwa majira ya saa moja usiku hajarudi. Usiku ule ukaisha. Kesho yake Mchungaji akaenda nyumbani kwa daktari walinzi wakasema hajarudi. Ofisini nako hayuko tangu alipopata ile simu. Siku nne zikaisha, hajulikani alipo.

Mchungaji akawaita wazee wa kanisa akawaambia naomba nibebe huu mzigo, kwani sijui nimueleze nani. Mama alikuwa na mtoto pekee na mume wake alishafariki. Hakuna kumbukumbu, akatoa taarifa vyombo vya habari akaona kimya. Siku ya tano akaenda serikalini kuomba kibali kuhifadhi mwili wa mama yule.

Kwa siku hizo tano daktari hakuonekana, si nyumbani wala kazini. Akamzika mama kwa heshima zote. Miaka mitatu baadaye, siku moja Mchungaji akiwa anapita na gari lake, akasikia mtu anamwita, mchungaji!

Naye yuko kwenye jalala amejaa uchafu sura haitambuliki. Mchungaji kushuka na kumwendea, binti akakimbia. Kwa mbali akawa anajitaja jina lake, kwamba ni mimi yule daktari fulani (akitaja jina). Mchungaji kumkimbilia hakumpata. Kumbe pale alipokuwa akiita mama hakurudi tena, ndio akawa kichaa wa jalalani. Wiki ijayo tuone kisa kinatufundisha nini. Je, una kisa?

***Ujumbe 0715268581.***

## NAWAZA KWA SAUTI

Na Salome Kitomari



# Mjadala wa nishati safi ulete suluhisho kushuka bei ya gesi

WIZARA ya Nishati imeandaa mjadala wa kitaifa wa siku mbili kuanzia Jumanne ijayo kujadili umuhimu wa nishati safi hasa wakati huu wa kasi ya mabadiliko ya tabianchi ambayo madhara yake yanaonekana dhahiri kwa sasa.

Mkutano huo utakuwa na mada za upatikanaji, upataji na unafuu wa nishati mbadala wa tungamotaka (kuni na mkaa), mtungi wa gesi ya kupikia kila nyumba, athari za kiafya zitokanazo na nishati ya kupikia na ustawi wa wanawake na ugharamiaji wa nishati safi ya kupikia.

Ni mjadala muhimu sana utakaofunguliwa na Rais Samia Suluhu Hassan, hasa wakati huu ambao dunia inakabiliwa na athari za mabadiliko ya tabianchi, huku waathirika wakubwa wakiwa nchi za Afrika ambazo mchango wao katika kuzalisha hewa ukaa ni mdogo sana.

Mjadala mkubwa kwa sasa nchini ni namna ya kupata nishati safi kwa bei nafuu. Wengi wanatamani kuachana na matumizi ya mkaa watumie gesi lakini bei yake imeendelea kupaa kila uchao.

Idadi ya tani za mkaa zinazoingia Dar es Salaam kila siku zinatosha kuonyesha kwa kiasi gani tunakwenda kuwa na jangwa kubwa siku za usoni na tayari Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), imeeleza kuwa mvua zilizotarajiwa kunyesha kwenye mikoa 14 hazitakuwapo tena, hivyo kutakuwa na ukame.

Aidha, athari zinaongezeka zaidi na sasa Dar es Salaam inakabiliwa na uhaba mkubwa wa maji kutokana na kupungua kwa maji katika Mto Ruvu na vyanzo vingine. Vyanzo vingi vinaendelea kukauka huku mifugo na viumbe vingine vikiwa katika hatari ya kupoteza maisha kwa sababu ya kukosa malisho.

Hali ni mbaya maeneo mengi ndiyo maana naona huu mjadala ni muhimu ili kupata suluhisho kwa mazingira yetu tunawezaje kuendelea na maisha katika wakati huu wa mabadiliko ya tabianchi.

Ninafurahi mjadala huu unafanyika siku chache kabla ya mkutano wa dunia wa mazingira (COP270) unaoanza Novemba 6, mwaka huu nchini Misri ambako kila nchi itatakiwa kueleza mipango yake ya kukabili mabadiliko ya tabianchi.

Wakati mwingine mawazo kutoka kwa wananchi wa kawaida kabisa yanaweza kuwa na suluhisho kubwa kwa kuwa wanaeleza kutokana na mazingira wanayoyaishi kuliko kufuata yale yanayotakiwa na nchi wahisani.

Mada za mjadala huu ni nzuri kama washiriki watakuwa na 'free mind' kwenda kujadili tulikotoka,tulipo na tunakokwenda kwa kuangalia kwa jicho la pekee siasa za duniani kwenye kila jambo hasa nishati.

Mathalani, tunasema mtungi wa gesi ya kupikia kila nyumba tujiulize nyumba za kijijini zinawezaje kumudu kununua gesi kwa ajili ya matumizi yao yote ya kutwa, kipato chao kwa mwezi ni Sh. gapi, gesi mtungi mdogo ni Sh.25, 000 na mkubwa 55,000 bado hajalipia usafiri.

Ni kwanini gesi iwe ghali nini kinaweza kushusha bei ya gesi ili kweli ipatikane kila nyumba, ni kwa nini nyumba inatumia gesi kwa vitu vidogo vidogo na kuwa na mkaa au kuni kwa ajili ya kupikia vya muda mrefu.

Ni kweli kuna athari za kiafya lakini watu wanafanyeje kupata nishati safi kwa bei inayowezekana kwa kila mtu na kwa urahisi zaidi je kuna uwezekano wa kuondoa gesi,wasambazaji wa gesi ni wafanyabiashara kutoka wapi na je wanaona Tanzania inavyoendelea kuwa jangwa?

**"Mada za mjadala huu ni nzuri kama washiriki watakuwa na 'free mind' kwenda kujadili tulikotoka, tulipo na tunakokwenda kwa kuangalia kwa jicho la pekee siasa za duniani kwenye kila jambo hasa nishati.**

Naamini hakuna mtu anataka kutumia nishati ngumu na yenye madhara ya kiafya kwake,kama atapata nishati safi kwa wakati na bei nzuri,hivyo ni muhimu mjadala wa kina wenye kuruhusu mawazo kinzani ukafanyika kuwezesha mabadiliko halisi.

Haitarajiwi mkutano huu kuwa kama mingine kwamba watu wanakutana, inatumika gharama kubwa, wanatoka na maazimio ambayo yanakwenda kubaki kwenye makabati hadi wakati mwingine kutakapokuwa na mkutano mwingine.

Tunatarajia pamoja na mambo mengine wataiwakilisha nchi kwenye COP27 waende na mawazo yetu, maamuzi yetu kwamba Watanzania tunaona suluhisho kwa kadri ya mazingira yetu ni hivi na hivi,tufurahi tunapopewa misaada ya mabadiliko ya tabianchi lakini nasi tuna maisha kwa kadri ya mazingira yetu.

# HARUSI



Wengi wamezoea gauni la harusi lazima liwe na rangi nyeupe, lakini unaweza kuwa mbunifu kwa kuwa na gauni la rangi nyingine. Hapa unajionea baadhi ya magauni yenye rangi nyekundu.

MITINDO



# Polo za wanaume wembamba

KATIKA kipindi hiki cha joto, mavazi mepesi ni kwa ajili ya kuufanya mwili kuhimili vuguvugu na kumfanya mtu kuwa na furaha wakati wote.

Wakati wa joto mgandamizo wa hewa huwa mkubwa na mwili unahitaji kupumua na hivyo mavazi mepesi yanafaa kutumiwa sehemu zote.

Shati la polo jepesi linapendwa kuvaliwa na wanaume katika kipindi hiki, na kuwa miongoni ya mavazi yaliyovunja rekodi kwa kupendwa kwa miaka michache.

Inaonekana urahisi wake wa kuchanganya na nguo tofauti hasa jinzi ni sababu tosha kwa wanaume kukimbilia kutumia.

Mbali na mashati yaliyoundwa kwa kiwango cha kawaida, sasa kuna yale yanayofaa wanaume wembamba.

Kuna aina tofauti ya mashati ya aina hii yakiwa na ukubwa na rangi tofauti.

Shati la polo nyembamba la wanaume linaweza kuvaliwa kwa urahisi kwa kila kizazi ambao wanaona umuhimu wa mtu kupendeza.

Mashati haya yanafaa hasa kwa mahitaji ya wanaume wembamba na wakati huo huo inahakikisha msisitizo mzuri wa miili yao.

UREMBO



USO BILA SUNZUA

# Fanya haya utaona matokeo

VISUNZUA ni vinyama vidogovidogo vinavyoota juu ya ngozi, hili ni tatizo la watu wengi kwa sasa, wanawake na wanaume.

Inasemekana visunzua hutokana na tatizo la homoni mwilini, unene uliopitiliza, kisukari na mabadiliko wakati wa ujauzito.

Watu wengi wanahangaika kutafuta tiba ya visunzua bila mafanikio.

Tutaelekezana namna ya kuondoa visunzua kwa njia ya asili ukiwa nyumbani kwako.

Nitakueleza vitu ambavyo unaweza kuandaa mwenyewe nyumbani kukabiliana na tatizo hili na likaisha ndani ya muda mfupi.

Vitu vingine ukivisoma hapa utastaajabu maana huwezi kufikiria vinaweza kuwa tiba.

**Kitunguu maji**

Kata vitunguu weka kwenye bakuli, changanya na maji ya tufaa, kisha viache vilowane usiku kucha, asubuhi chukua vitunguu bandika kwenye visunzua kisha funga vizuri na plasta visitoke acha kwa saa 4 hadi 5. Fanya hivi kila siku kwa muda wa wiki moja utajipenda.

**Kitunguu saumu, baking soda na limao**

Menya kitunguu saumu, kisage kiwe laini changanya na baking soda kijiko kimoja kisha changanya na limao. Paka mchanganyiko kwenye sunzua ukiweza funga na plasta, kaa kwa masaa mawili hadi matatu osha.

Paka mara tatu kwa siku. Ni vizuri usiku ukilala nayo. Baada ya muda mfupi utapata matokeo mazuri.

**Asprin**

Aspirin dawa ambayo humezwa kwa kutuliza maumivu, lakini inapondwapondwa upate unga kisha kuichanganya unapata dawa nzuri ya kuondoa sunzua.

Paka kwenye sunzua mara tatu hadi nne kwa siku na baada ya wiki utaona mabadiliko.

**Rangi ya kucha**

Rangi siyo tu urembo wa kucha, hapa rangi inafanya kazi nyingine. Paka rangi kwenye sunzua mara tatu hadi nne kwa siku. Usiku unashauriwa kulala nayo na ubandue asubuhi. Wiki moja tu utaona mabadiliko makubwa.

**Ganda la Ndizi**

Bandika sehemu ya ndani ya ganda la ndizi na usugue kwenye sunzua mara nyingi uwezavyo kwa siku .Ili upate matokeo mazuri bandika plasta na uiache kwa muda mrefu.

MAPISHI

Na Mary Geofrey

# Supu ya pweza











WENGI tumezoea kunywa supu ya pweza kwenye migahawa na maeneo ambako wauzaji wanaweka kama kwenye vituo vya daladala na kwenye mikusanyiko.

Leo kwenye safu ya mapishi tunaelekezana namna ya kuandaa supu hii ambayo inatajwa kuwa na faida nyingi mwilini ikiwamo kuongeza maziwa kwa mama anayenyonyesha.

**Mahitaji**

Pweza kilo moja, chumvi kijiko kimoja cha chai, tangawizi mbichi iliyosagwa kijiko cha chai kimoja, kitunguu saumu iliyosagwa kijiko cha chai na masala kijiko kimoja cha supu.

Mahitaji mengine ni pilipili mbuzi ili ipate kiharufu kizuri ikichemka, maembe mabichi na ndimu au limau ili kuongeza ladha ya supu yako.

**Namna ya kutayarisha**

Osha pweza kisha mkatekate, mtie viungo vyote ulivyotayarisha na chumvi muache nusu saa ikolee viungo.

Mtie ndani ya sufuria bila maji mfunike kisha weka jikoni, atatumbuka maji mwenyewe kwa moto wa kiasi paka awe rangi ya damu ya mzee.

Akishaiva kwa rangi hiyo ongeza maji saizi ya supu unayotaka, weka na maembe yako yachemkie.

Ukiona imeiva tia kipande cha ndimu au limau hapo itakuwa tayari kwa ajili ya kunywa ikiwa ya moto ili kuongeza afya mwilini.

## MAISHA NI NYUMBA
Na Elizabeth Zaya

# Namna kabati la vyombo kupendeza



BILA shaka kabati la vyombo ndio fenicha muhimu kwenye chumba cha chakula kutokana na kuchukua nafasi kubwa kwa mwonekano.

Kwa kawaida muundo wa kabati la vyombo una sehemu mbili. Ipo sehemu ya juu yenye vioo vyombo vinaonekana vilivyotandazwa.

Sehemu ya pili ya kabati ni ile ya chini yenye droo na kabati vyombo havionekani.

Unapoamua kupendezesha kabati la vyombo eneo la vioo linakupa fursa kufikiri tofauti jinsi ya kuonyesha vyombo.

**1:** Hatua ya kwanza ya kupendezesha kabati la vyombo ni kuondoa kila kitu na kuanza upya. Baada ya hapo chambua vyombo vizuri ambavyo ungependa vionekane.

**2:** Panga sahani pembeni huku katikati ukiweka vyombo vingine kama majagi, glasi na vikombe vichache vile vyenye mvuto tu.

**3:** Baada ya kusambaza vyombo vyako vya kuvutia kwenye eneo la vioo la kabati, kinachofuatia ni kuweka mapambo mengine kama vile picha za familia.





# Sababu nyumba kuvuja muda mfupi baada ya kujengwa







KUWA na nyumba bora na imara ni ndoto na furaha ya kila mtu anayemiliki au anayetarajia kumiliki nyumba hiyo.

Lakini inapokuwa kinyume na matarajio ya kumiliki nyumba ya vigezo hivyo, moyo huinama japokuwa wakati mwingine hali hiyo inasababishwa na kukosea uchaguzi wa wataalamu wa ujenzi wa nyumba husika ambao hujenga chini ya kiwango.

Mtaalamu wa masuala ya ujenzi, Andrew Kitale, anazungumzia baadhi ya makosa ambayo hufanyika wakati wa kutafuta watalaamu wa kujenga nyumba, hivyo kuchangia kutokea matatizo muda mfupi baada ya nyumba kujengwa, ikiwamo kuvuja.

Anataja sababu mbalimbali zinazochangia baadhi ya nyumba kuvuja muda mfupi baada ya ujenzi kuwa ni pamoja na matumizi ya vifaa vya ujenzi vya hali ya chini ambavyo baadhi ya watu hufanya hivyo kwa kudhani wanaokoa pesa.

Sababu nyingine, anasema baadhi ya vifaa vinavyotumiwa na mafundi wakati wa kuezeka huwa si rafiki kwa nyumba, hivyo kudhoofisha kifuniko cha paa ambacho baadae hutengeneza ufa na kupitisha maji.

Mbali na sababu hizo, pia anasema paa la nyumba linaweza kuharibiwa na upepo hasa kama halikuezekwa kwa utaalam mzuri na hivyo kuvuja.


Sababu nyingine anasema ni muundo wa paa lenyewe pamoja na makosa yaliyofanywa wakati wa kuezeka na kwamba kwa makosa hayo ya kuvuja kunaweza kutokea hata ndani ya mwaka mmoja baada ya ujenzi wa nyumba husika.

Nyingine anasema ni ufungaji mbaya wa paa wakati wa kuezeka na kwamba kasoro kama hiyo huonekana haraka ndani ya wiki chache baada ya nyumba kuanza kutumika.

"Paa linaweza kuvuja kwa sababu ya ukiukaji wa matumizi ya teknolojia ya ujenzi. Kwa mfano, kitaalamu unatakiwa kuweka nyenzo za kuezekea kwa tabaka tatu, wewe unaweka tofauti na hapo na makosa mengine madogo yanayofanana na hayo yanayofanywa wakati wa kuezeka," anasema.

Anashauri kwamba njia ya kuepuka paa lako lisivuje ni kuwa makini kuchagua wataalam wa kukuezekea, kutumia vifaa bora bila kujali gharama, kufuata kanuni zote za uezekaji na kukagua paa lako mara kwa mara angalau mara mbili kwa mwaka na kuondoa vitu vyote ambavyo hutuama juu yake ambavyo kwa namna moja ama nyingine hutengeneza nyufa hususani vyuma na vitu vizito.

# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2022
SMS - 0621 412 879
KORITINI
KWANI HAYA MAVAZI YANA-HAMIRA? MAANA KILA ANAYEVAA ANAUMUKA
VAA NA WEWE
JUKWAANI
AFANDE HUYU NIMEMFUMANIA NA MKE WANGU
HUYU KAOA DEMU WANGU TULIKUWA SIJAMUACHA
SHERIA ILIBIDI MRUSHE SHILINGI, LAKINI NYIE MNATIANA MAGUMI YA KIJAMBAZI MCHANA!
MIE NGOSHA UNANIPIMIA HAKA KAUGALI KAKIZARAMO KWELI?
SAMAHANI MTANI 'VUMILIAVUMILIA' NIMETIA HAMILA MUDA SI MREFU USUBIRIE KIDOGO
NYIE KINA NANI MPAKA MNAJADILI MAMBO YA KIJEDA?
NENO LISHAZUA NENO
HASHUKI MTU MPAKA NIJUE DHAMIRA YENU SIVYO KAMBINI TUKAJUANE
KA'MKUBWA SIJAONGEA MIE NAUMWA JINO
AFANDE BABA NIMEFIWA MIE MAREHEMU KESHAAMKA
KONDA NISHUSHE HAPO HAPO
WE'USINIPONZE UTOKEE DIRI-SHANI KWANI MLANGO AKUNA AU NKUSEMEE?
NJAA BILA KUIFANYIA MAZOEZI ITAKUUA UNAOZA UMESIMAMA WIMA
MTIHANI WOTE ULIKUWA SIMPO SANA MAJIBU 'YA KUBETI'
NILIDHANI ZILE 'ANA,ANADOO' UNAIMBA TU!
*KINYUNYIZO CHA LEO...
...UZURI WA GEREZA ULIONE KWA NJE

# Ukraine yatangaza nchi kuwa gizani

**KYIV**, UKRAINE

SERIKALI ya Ukraine imeonya watu katika mji mkuu wa Kyiv kutarajia kukatwa kwa umeme kwa muda mrefu, kwa zaidi ya saa nne kutokana na mashambulizi ya Russsia yanayoangamiza miundombinu ya nishati.

Kukatika kwa umeme kunaikumba pia mikoa ya kati ya Ukraine, pamoja na jiji la Dnipro.

Rais Volodymyr Zelensky alisema takriban watu milioni nne wameathiriwa, lakini alisisitiza mizinga haitawamaliza.

Mwezi huu Russia ilirusha makumi ya makombora na ndege zisizo na rubani zilizotengenezwa na Iran.

Miundombinu ya nishati ya Ukraine inakumbwa na mashambulizi ya anga, Rais Zelensky alisema theluthi moja ya vituo vya kuzalisha umeme nchini humo vimeharibiwa.

"Eneo la Kyiv limepoteza asilimia 30 ya uwezo wake wa nishati, kutakuwa na katizo la umeme kuliko ilivyokuwa hapo awali," alisema mkurugenzi wa kampuni binafsi ya umeme ya DTEK, Dmytro Sakharuk.

Kukatika kwa umeme kutazuia matumizi ya taa za barabarani na umeme.

EU yazuia mali ya Russia

Mali za Russia zenye thamani ya euro bilioni 17 imezuiliwa na Umoja wa Ulaya, tangu kuanza kwa vita.

Kamishna wa Haki wa EU, Didier Reynders alisema katika mahojiano na chombo cha Habari cha Funke.

Hatua hiyo inatekelezwa kama sehemu ya utekelezaji wa vikwazo na umoja huo.

"Kwa sasa, mali za watu 90 zimetaifishwa zenye thamani ya zaidi ya euro bilioni 17 katika nchi saba wanachama wa EU ikiwa ni pamoja na euro bilioni 2.2 nchini Ujerumani". alisema Mnamo mwezi Julai, Reynder alitaja kiasi kingine cha euro bilioni 13.8, ambapo zaidi ya euro bilioni 12 ilichangiwa na nchi tano za EU.

Idadi ya nchi imeongezeka hadi saba, kati ya mali iliyozuiliwa ni boti za kifahari, majengo, na akaunti za pesa.

Wanasiasa wa Ukraine walidai mara kwa mara kwamba mali iliyozuiliwa itumike kujenga nchi yao baada ya vita, kama ilivyonukuliwa na DW.

Katika hatua nyingine, Marekani imeipatia Ukraine kifurushi kipya cha msaada wa kijeshi kiasi cha dola milioni 275.

Hayo yalisemwa na naibu msemaji wa Ikulu ya Marekani, Sabrina Singh, katika mkutano mfupi.

Alisema msaada huo ni pamoja na risasi za ziada kwa mifumo ya roketi ya kurusha ya HIMARS, makombora 500 ya usahihi wa hali ya juu na makombora 2,000 ya RAAMS kwa mizinga 155 mm, makombora 1,300 ya kukabiliana na vifaru, magari 125 ya kijeshi ya Humvee, silaha ndogo ndogo na risasi milioni 2.7 na antena 4 za mawasiliano ya satelaiti.

"Tangu kuanza kwa utawala wa Biden, Marekani imetenga dola bilioni 18.5 kama msaada wa kijeshi kwa Ukraine,"alibainisha.

"Tumepata silaha zaidi za HIMARS, makombora na vifaa vingine. Tunashukuru washirika wetu," alisema mkuu wa ofisi ya rais, Andriy Yermak kupitia mtandao wa telegram.

***BBC***



Wanajeshi wa Ukraine wakirusha kombora kwenye mstari wa mbele wa vita katika mkoa wa Kharkiv. **PICHA: REUTERS**

# UN yatabiri mabaya Palestina

**NEWYORK,** MAREKANI

MJUMBE wa Umoja wa Mataifa kwenye eneo la Mashariki ya Kati,Tor Wennesland amesema 2022 huenda ukawa mwaka mbaya zaidi kwa Wapalestina katika Ukingo wa Magharibi.

Amesema athari hiyo imeanzia tangu Umoja huo ulipoanza kufuatilia matukio ya vifo mnamo mwaka 2005, huku akitoa wito wa kuchukuliwa hatua za haraka kuzuia kutokea kwa hali ya uhasama.

Wennesland aliliambia Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa kuwa kuibuka na kuongezeka kwa hali ya kukata tamaa, hasira na mvutano vimesababisha matokeo ya vurugu na vifo ambavyo imekuwa vigumu kuvidhibiti, huku watu wengi hasa Wapalestina wakiuawa na kujeruhiwa.

Mjumbe huyo alisema hali hiyo imesababishwa na miongo kadhaa ya vurugu na kutokuwepo kwa muda mrefu mchakato wa mazungumzo.

Zaidi ya Wapalestina 125 wameuawa tangu kuanza mwaka huu katika makabiliano na Israel katika Ukingo wa Magharibi na Jerusalem Mashariki.

Alisema juhudi zinapaswa kuelekezwa katika kuanzishwa kwa duru mpya ya mazungumzo kati ya Israel na Palestina.

***DW***

## Iran yatoa onyo kwa waandamanaji

**TEHRAN,** IRAN

MKUU wa kikosi cha Walinzi wa Mapinduzi cha jeshi la Iran, Hossein Salami, amewaonya waandamanaji kuwa jana itakuwa siku yao ya mwisho kuingia mitaani na kuitaja kuwa ni siku ya mwisho ya ghasia.

Iran imekumbwa na maandamano makubwa tangu kifo cha Mwanamke wa Kikurdi Mahsa Amini mwenye umri wa miaka 22 ambaye alifariki mwezi uliopita akiwa chini ya ulinzi wa polisi wa maadili.

Jana, picha za video kwenye mitandao ya kijamii ziliwaonyesha waandamanaji wakitoa wito wa kuuawa Kiongozi Mkuu wa Iran Ayatollah Ali Khamenei na wanamgambo wa Basij, ambao wamechangia katika ukandamizaji dhidi ya waandamanaji.

Mashirika ya kutetea haki za binadamu yalisema waandamanaji 250 wameuawa huku maelfu ya wengine wakikamatwa nchini kote.

## Ufilipino yatangaza idadi mpya ya vifo

**MANILA,** UFILIPINO

SERIKALI ya Ufilipino imebadili takwimu za idadi ya waliokufa kutokana na kimbunga kilichoipiga nchi hiyo juzi na kusema watu 45 pekee walipoteza maisha.

Mapema jana ofisi ya ulinzi wa raia iliripoti kwamba watu 72 walikufa, 14 hawajulikani walipo na wengine 33 walijeruhiwa.

Maofisa wa ulinzi wa raia walikiri kuwa timu za uokoaji zilizotumwa kusini mwa nchi hiyo zilikosea katika kuripoti, na hivyo kusababisha vifo vingine kuhesabiwa mara mbili. Mkuu wa vikosi vya ulinzi wa raia Rafaelito Alejandro, alithibitisha takwimu hizo katika mkutano na waandishi wa habari huko mjini Manila, akisema miili 40 ilipatikana katika eneo la kusini la Mindanao.

Kutokana na mazingira yake ya kijiografia kuwa eneo tete la uwezekano wa kulipuka kwa volkano na kutokea matetemeko ya ardhi, Ufilipino inakabiliwa na takriban vimbunga na dhoruba kiasi cha mara 20 kila mwaka.

***DW***

MAKALA

# ULIPO HUSTAHILI KUWAPO



Na Magabilo Masambu

MAISHA ni fumbo lenye siri kubwa kama kilivyo kifo. Inawezekana una ugonjwa ambao unajua tu kwa vyovyote vile utafariki dunia lakini ni lini, saa ngapi na wapi hilo analijua Mwenyezi Mungu. Ukifikiria zaidi utagundua kwamba palikuwa na sababu ya mambo haya mawili makubwa kufichwa na kuwa ya siri.

Inawezekana kama tungelikuwa tunajua moja kwa moja siri hizi basi tungelitenda uhalifu mkubwa sana hapa duniani. Ni kweli kwamba kila mtu anajua siri ya mafanikio yake, lakini siri hiyo inajulikana pale utakapokuwa umeshafanikiwa na hiyo haitakuwa siri tena, kwa sababu tayari inajulikana hata kama si kwa watu wengi.

Kuna watu ukiwatazama utagundua kwamba wako sehemu wasizostahili kuwapo. Unaweza kuwa kwenye siasa ukawa kwenye chama kisicho na misingi uliyo nayo, unaweza kuwa mwandishi wa habari kumbe ulitakiwa kuwa daktari. Unaweza kuwa mwalimu kama mimi lakini kumbe ulitakiwa kuwa mwandishi wa habari wa aina yake na kadhalika.

Sababu za kuwa mahali ambapo hustahili zinaweza kuwa nyingi. Moja, kuna watu wanaweza kuwa kila mahali, wanaitwa 'multiple talented'! Ukipelekwa kokote unafaa na unafanania na hapo. Wengine wapo walipo kwa sababu hawakupata mwongozo wakati wa kuamua kuwapo huko. Wengine labda kipato, alikwenda mahali kwa sababu ndipo kipato chake kilifaa kwa wakati huo lakini wengine mkumbo kwa sababu wenzangu wamekwenda huku nami ngoja niende.

Ikishatokea hivyo, hakuna sababu ya kulalama na kulaumu sana. Ukishagundua kwamba njia uliyopitia haitakufikisha mahali unapopataka, basi huna sababu ya kuendelea kuwa huko kwa sababu kwa namna yoyote ile hutaweza kufika unapopataka hata kama unafanya kwa ufanisi lakini nafsi yako ipende. Jambo la ajabu ni kwamba wako wanaogundua kuwa mahali walipo sipo wanapostahili, lakini hawafanyi mabadiliko. Badala yake, bado ama wanaendelea kujilaumu au wanawalaumu wazazi wao ingali na wao ni wazazi.

Kuna wazazi leo wanawaeleza watoto wao kwamba maisha waliyo nayo yalisababishwa na wazazi wao (babu na bibi). Yaani unataka kujisafisha kwa watoto kwa kuwatupia lawama wengine kwa udhaifu wako wa kutopambana kuyafikia malengo yako. Unataka watoto wako wamchukie babu yao hilo litasaidia nini? Unachokizungumza hakiwezi kurudi nyuma hata kama inawezekana yeye alikuwa chanzo. Lakini yafaa nini kuwaeleza unataka wakuonee huruma na maelezo hayo yatumike kama utetezi wa kutowakamilishia mahitaji yao ya msingi kama baba wa familia.

Kwa wale ambao hawajaamua mwelekeo wa maisha yao uweje, ni muhimu sana kabla ya kuamua uwe umefanya uchambuzi wa kutosha. Kama ni chama cha siasa unachotaka kuingia, lazima uwe na uhakika kwamba kitakufikisha kwenye malengo yako na ya kitaifa. Kinachowafanya baadhi kuhamahama vyama vya saisa, wakati mwingine ni kutokana na kwamba wakati wanajiunga hawakuwa wamejiridhisha vyema. Wako ambao wakishaingia wanapata taabu kutoka lakini moyo wao ukiwa kwingine.

Dr. Shuller anasema 'the failure is not final'. Kushindwa jambo fulani si mwisho, hivyo unaweza kushindwa kwa sababu mahali ulipo si sahihi kwako. Jambo ambalo kwa wengi wetu ni gumu ni kubadili baada ya kugundua kwamba walipo si mahali sahihi kwao, wanaona kuanza upya ni kupoteza muda, lakini wanakubali kupoteza muda kuendelea na njia ambayo haitawafikisha. Ikiwa tutafanya hivyo basi tutayafikia malengo tukiwa tumechoka sana.

Bahati mbaya tuliyo nayo Tanzania pengine na Afrika nzima ni tabia ya watu kushangaa mtu kufanya kazi kwenye taaluma ambayo hakusomea. Yaani tunataka mtu aliyesomea uhandisi wa umeme na mitambo asiwe mwandishi wa habari, mfanyabiashara na kadhalika.

Ni kweli kwamba kuna baadhi ya taaluma huwezi kufanya kazi kama hujasomea mfano utabibu wa binadamu, lakini bado kama utakuwa wewe ni mtaalamu wa fani fulani njiani ukagundua kwamba ulifaa kuwa daktari wa binadamu na unaendelea lakini wewe ni mwalimu wa Kemia na Baolojia, basi huna budi kutafuta utaratibu wa kuwa daktari kwa kujiendeleza. Usibaki tu unasema nilitamani kuwa daktari, nafasi unayo na wala usitazame muda kwamba umeenda inawezekana ukiwa daktari itakulipa muda wako wote uliopoteza kwenye fani yako ya mwanzo.

Kwa ufupi, chukua hatua sasa. Usiendelee kujuta kwani kadri unavyoendelea kulalamika na kujilaumu ndivyo utendaji wako katika kazi unayofanya unaendelea kufifia, kwa hiyo itafika wakati hata kazi yenyewe itaonekana huiwezi hata kama ulifaulu vizuri masomo yake.

Wengi wanajiuliza je, ni umri gani wa kubadili fani au kada? Nasema hakuna muda maalumu, maana kuna wengine wakistaafu wanafanya kile walichokuwa wanakipenda kwahiyo unakuwaje muoga wa kubadili mapema?

Uzoefu unaonyesha wengi waliobadili fani katika umri mkubwa, wamefanikiwa sana katika fani mpya kwa sababu wanakuwa wamefanya uchambuzi wa kutosha labda kama imetokea umebadili kwa kufuata mkumbo au kushauriwa badala ya kuamua wewe binafsi. Amua sasa utafanikiwa usiogope, maana mafanikio yako yako kule unapopawaza kuliko hapo ulipo.

Ukiwa CCM ukaona CHADEMA itakufanya uyafikie malengo yako, hamia haraka bila kujali wanaokuzunguka watasemaje na ukiwa Chadema ukaona CCM itakuwa njia sahihi hamia vile vile. Wanaokuzunguka watakushangaa kwa muda mfupi tu kisha wakishaona utendaji wako watasahau kwani walikupenda wewe hawakupenda chama labda wewe ndiyo ubadilike.

***0689157789***
***magabilomjalifu@gmail.com***
***SJMC-UDSM***

BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# Kasheba alipotabiri kifo chake kwenye 'Dunia Msongamano' na 'Yellow Card'



Na Adam Fungamwango

"HATA nikifa sitomaliza vifo wala sitojaza ardhi, nitakwenda kwenye kaburi langu mwenyewe, usiwe na wasiwasi na wewe lako lipo, kwa sababu na wewe ni marehemu mtarajiwa, linakusubiri. Amekufa Masiya, wamekufa Mitume na Masultani, watawala wenye sifa, nguvu na pesa nyingi, sembuse mimi na wewe viumbe dhaifu, jamani tuhurumiane."

Ni maneno mazito yaliyotoka kinywani mwa mwanamuziki maarufu nchini tangu miaka ya 1970 alipofika nchini kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo hadi alipofariki mwaka 2004, Freddie Ndala Kasheba.

Mwanamuziki huyo aliyejizolea umaarufu mkubwa si kwa utunzi tu na kupiga gitaa la solo, bali pia ndiye mwasisi wa kupiga gita la nyuzi 12, ambalo mashabiki wake walilipachika jina la dazani, wengine wakaenda mbali zaidi wakalibatiza jina la kombora.

Awali, hakukuwa na mwanamuziki yeyote nchini aliyekuwa anajua kama kuna aina hiyo ya gita, lakini alipoingia kwenye bendi ya Orchestra Safari Sound baada ya Kikumbi Mwanza Mpango, 'King Kiki' kumaliza mkataba wake, alitaka alete kitu tofauti, ndipo alipowashangaza wengi kwa kuja na gita lenye nyuzi 12 badala ya sita kama ilivyo kawaida.

Kasheba aliyezaliwa 1946 na kufariki dunia Oktoba 22, 2004 jijini Dar es Salaam, akiwa na miaka 18 sasa chini ya tumbo la ardhi, ana historia ndefu kwenye muziki wa Tanzania na amekuwa na mchango mkubwa kwani huwezi kuuzungumzia muziki wa nchi hii bila kutaja mtu huyu aliyejizolea sifa na mashabiki kemkem.

Alifika nchini mara ya kwanza nchini mwanzoni mwa miaka ya 1970 akiwa na Orchestra Fauvette ambayo baadaye ilijulikana kama Safari Nkoi akiwa na King Kiki, walipoondoka na kurudi mara ya pili wote walijiunga na Orchestra Safari Sound (OSS) ya Masantula Ngoma ya Mpwita. Lakini hakukaa sana akamuachia Kiki yeye akaenda zake nchini Burundi.

Kikii alipomaliza mkataba na OSS, mmiliki wa bendi hiyo, Hugo Kisima, alimrudisha nchini Kasheba kushika hatamu ya uongozi. alibadilisha mtindo kutoka Masantula Ngoma ya Mpwita uliovuma kuanzia mwishoni mwa miaka ya 1970 na kubuni wa kwake, akauita Dukuduku.

Leo tunachoangalia ni nyimbo mbili alizozitunga baada ya kuzushiwa kifo mara mbili kwa miaka ya tofauti. Mwaka 1984 aliumwa na kulazwa kwenye Hospitali ya Aga Khan, Dar es Salaam. Taarifa ambazo si za kweli zikasambaa kwamba amefariki dunia. Hata baadhi ya bendi zilitangaza kifo chake kwenye kumbi ambazo zilikuwa zinapiga.

Siku mbili baadaye ilitokea picha yake kwenye gazeti la Mfanyakazi akiwa ameketi kwenye kitanda cha hospitali, juu kukiwa na maandishi 'Sijafa'. Alipona na alipotoka akatunga kibao kiitwacho 'Dunia Msongamano' ambacho kina mashairi kama yafuatavyo;-

"Mawazo yamenijia leo aliyokuwa mzee wangu akisema, dunia ni msongamano wa watu wenye akili tofauti, ukitaka kuishi vyema fikiri kabla ya kujibu, jifunze kwa waliwengu, waliwengu wajifunze kwako, dunia ni kuona mambo, halafu kuyasahau.

"Mateso nimeshayapata, matatizo mengi yamenikuta, furaha nyingi nimeshaona, maisha nusu nimeshafanya, naelekea uzeeni sasa lazima niwe na utulivu, sababu kuishi kwingi, ni kuona mengi, kuelimisha wataobaki ili waishi kwa heshima."Dunia msongamano kasema baba, nimeyaona leo nakubali mimi. Wengine hupendelea kufurahia, wanaposikia fulani kafa oo kufa kwa binadamu hupangwa na Mungu namuomba mwenyezi anipe maisha."

Walimwengu hawakuishia hapo. Mwanzoni mwa mwaka 2000 alikwenda kwao Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) kusalimia. Lakini zikaja taarifa za kizushi kuwa yuko hoi kwa kuumwa Kinshasa, wengine wakasema amefariki dunia. Ni taarifa zilizosambaa na kutangazwa sana kwani zililetwa na watu wa kuaminika.

Aliporejea nchini na kukuta anaitwa marehemu, alionekana kukasirika, akachukua gitaa lake kombora na kutunga wimbo wa 'Yellow Card.'

Ni wimbo ambao aliimba peke yake na gitaa yake tu. Hakuishirikisha hata bendi yake ya Zaita Musica. Akaimba wimbo wenye maneno makali na hisia kali sana.

"Zamani niliimba leo naimba dunia maajabu, Zamani niliimba leo naimba dunia matatizo, miaka ya 1980, walitangaza nimekufa, mwaka 2000 wakatangaza niko mahututi Kinshasa.

Nimeshazoea, imekuwa ni kawaida kila kukicha, wanamaarufu wana matatizo. Magonjwa yote ya dunia nimepachikwa mimi, wafurahi wao wenye uhakika wa afya njema, wataishi milele.'

'Wakishakutana kwenye makontena kwenye vistoo kwenye kiti moto, ajenda maisha ya watu. Wakishakutana chini ya mwarobaini kwenye supu ya utumbo, mazungumzo yote utumbo. Fulani amekwisha, si lolote si chochote gari hana, mke kamkimbia kaenda zake Ulaya. Yote nakubali namuachia Mungu aliyeniumba, anajua mwisho wa maisha yangu. Kama dhidi yao nimecheza rafu, Mungu ndiye mwamuzi atanipa kadi 'Yellow Card', itakuwa ni onyo, kama ni nyekundu niondoke duniani, yote ni ya Mungu.

"Jua linawaka mjini, nimepiga tai na shati jeupe natembea taratibu naogopa jasho wao wanasema siku hizi siwezi kutembea nimechoka. Eti jamaa yuko hoi hamalizi mwaka anaondoka huyo, tumpeleke tumpeleke. Mwezao anaumwa wao wanacheka eti alikuwa na mali wache akome, kuzika wanashindana kuchanga tiketi ya ndege ipatikane haraka wakazike kijijini kwa sababu wakizika mjini wataota jinamizi.

"Hata nikifa sitomaliza vifo wala sitojaza ardhi, nitakwenda kwenye kaburi langu mwenyewe, usiwe na wasiwasi na wewe lako lipo, kwa sababu na wewe ni marehemu mtarajiwa, linakusubiri.

Amekufa Masiya, wamekufa Mitume na Masultani, watawala wenye sifa, nguvu na pesa nyingi, sembuse mimi na wewe viumbe dhaifu, jamani tuhurumiane."

Nyimbo hizo mbili kwa mujibu wa baadhi ya wachambuzi wa masuala ya muziki wanasema zilikuwa ni kama kutabiri kifo chake. Alifariki dunia Oktoba 22, 2004 na kuzikwa kwenye makaburi ya Kinondoni, Dar es Salaam.

# HADITHI

HAKUNA aliyeamini alichokisikia, wala aliyeamini macho yake kwa kile alichokiona. Awali kulikuwa na vigelegele, ngoma, bashasha na furaha tele kwa watu wote waliohudhuria harusi hiyo. Bwana harusi Jerry Mohamed aliliongoza kundi la ndugu, rafiki na jamaa kutoka Dar es Salaam kwenda Kibaha kwa Mathias mkoani Pwani kwa ajili ya kufunga ndoa na mwanamke Vayajo waliyekubaliana kuoana. Mabasi, magari, bajaji, bodaboda, vyote vilimiminika kwenda huko kila mmoja akiwa na furaha tele. Kilichotokea ndicho kilicholeta mkasa mzima kwenye sakata hili la aina yake. Nini kimetokea? Kwa nini? Sababu ni nini? Na baada ya hapo nini kinaendelea? Kila nakala yako ya Nipashe itakupa majibu ya kisa hiki cha kushangaza.

# Harusi imevunjika-3

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

ALIISOMA na kuirudia mara tatu.Ilikuwa ni simu ya babu yake Vayajo. Ni mzee mwenye akili nyingi, uwezo wa kutatua jambo na alikuwa anaelewana naye sana. Kifupi alikuwa ni rafiki yake mno, kuliko hata wazazi wa msichana huyo.

Jerry alifikiri kama ende au asiende. Aibu aliyoipata siku ile kila mtu anamuangalia yeye, leo arudi tena Kibaha 'akajichoreshe' "Hapana" alijiambia.

Akakumbuka pia aliapa wakati anarejea kuwa hatorudi tena kule, kwa sababu atakapokuwa anaona madhari ya eneo lile la Kibaha atakuwa anamkumbuka Vayajo na madhila yote aliyomfanyia. Dakika moja baadaye akakumbuka kitu.

Akakumbuka mara ya kwanza alipopelekwa Kibaha na Vayajo, siku za mwanzo tu za penzi lao baada ya kukutana maeneo ya Chang'ombe Dar es Salaam na kutokea kupendana alimwambia kuwa huko anaishi kwa dada yake, lakini kwao hasa ni Kibaha.

Kutokana na kuwa kwenye lindi la mahaba ya mwanzoni, Vayajo aliamua kumpeleka nyumbani kwao. Akamhakikishia kuwa hakuna kitu chochote kitakachomtokea, japo Jerry alimwambia haitokuwa vema kwenda nyumbani kwao wakati wazazi hawamfahamu na hajatambulishwa rasmi.

Siku zote penzi ni upofu, pamoja na kujua yote, lakini alilaghaiwa, akapelekwa. Akakaribishwa vizuri, mama hakuwa na tatizo sana. Ingawa hakutambulishwa, lakini jinsi alivyofika pale na binti yake, akajua kuna namna tu hapa.


Baba pia alivyorudi kwenye mishughuliko yake, akamkuta mgeni, wakasalimiana, akamwita mkewe chumbani wakaongea, Vayajo naye alikuwa ametoka kidogo kusalimia shoga zake aliporejea, naye akaitwa.

Ingawa hakufukuzwa, lakini alichokisikia kwa mbali chumbani ni kufokewa kwa mpenzi wake kama mtoto mdogo kuwa kwa nini anawaletea mtu bila kuja kujitambulisha rasmi kwanza kama mila na utamaduni unavyotaka.

Jerry anakumbuka Vayajo alitoka chumbani, akamwambia waondoke bila kuonyesha kama amechukia, akatii amri.

Alijua wanaondoka kurudi Dar, lakini walikwenda sehemu nyingine ambayo haikuwa mbali sana na hapo.

Ilikuwa ni nyumba ya mzee Mbegu babu yake Vayajo. Wakakaribishwa vizuri. Binti akamchukua babu yake ndani na kumueleza kilichotokea. Alimsikia kwa mbali babu akisema "Huyu mume mwenzangu atakaa hapa, atalala hapa mpaka atakapoondoka. Na hilo la baba yako niachie mimi, yule nimemzaa mwenyewe hawezi kunishinda."




"Hadi leo si mimi, baba yake wala mama yake anayejua yuko wapi. Ni wiki ya tatu sasa hii hatujapokea simu wala taarifa kutoka sehemu yeyote ile."

Mzee Mbegu ndiye aliyekwenda na kusawazisha mambo kiasi cha kukubaliwa sasa na baba Vayajo kuishi pale kama mkwe ingawa hajajitambulisha. Akawa anakwenda kula chakula cha mchana na jioni kwa wakwe zake, halafu anakwenda kulala na babu, Vajayo akilala nyumbani kwao.

Babu aliimaliza kesi hiyo, ila akaambiwa siku akiondoka, basi atakapotaka kurejea pale aje na mshenga alete barua ili wamtambue rasmi, halafu watajua wenyewe ndoa itakuwa lini.

Ndiyo maana hadi leo hii akikumbuka hilo, anamheshimu sana mzee huyo na ndiye aliyemwita.

Baada ya kukumbuka hilo, akabadili mawazo kwa heshima ya mzee hiyo. "Nitakwenda kumsikiliza."

****************************************

"Kwanza kijana pole kwa yote yaliyokukuta." Ilikuwa ni sauti ya mzee Mbegu iliyomalizika na kikohozi kizito. Alikuwa anavuta sigara kali ambayo staili yake ilikuwa ikimshangaza sana Jerry.

Upande ule aliouwasha ndiyo alikuwa ameugeuza na kuutoa mdomoni, na upande uliokuwa nje ni ule ambao hauna moto.

Sigara hiyo haikuwa na kishungi, badala yake pande zote zilikuwa ni kama zile sigara za kawaida upande ambao hauna kishungi.

"Ahsante babu." Akajibu kwa kifupi, lakini kwa sauti yenye maumivu makali. Jerry alifika Kibaha kwa staili ya aina yake. Kutokana na aibu kubwa aliyoipata kwenye sherehe ambayo aliyepaswa kuwa mkewe alitoweka, hakufika mchana. Alitinga kwenye kijiji cha Msangani mida ya saa 1:00 usiku, giza likiwa limeingia.

Alikuwa amevaa kofia iliyoziba sura yake, huku yeye mwenyewe akiwa amebakisha macho tu ya kumuwezesha kuona anakokwenda.

Alikuwa amevaa jinzi lililopauka na fulana ya mikono mirefu. Alikuwa akitembea mwendo wa haraka haraka bila kumtazama yoyote, hivyo kama walikuwa wakimwangalia au la.

"Hivi vitu huwa vinatokea kwenye maisha, kwa hiyo si wewe tu ambavyo vimekukuta, au utakuwa wa mwisho. Mradi tu unaishi kwenye hii dunia utakutana navyo na utakuja kuona wengine pia wanakutana navyo. Wakati huo wewe utakuwa kwenye dunia nyingine kabisa."

"Ni kweli mzee, lakini inauma sana na imeshakuwa dua kubwa sana kwenye maisha yangu..."

"Sawa najua kijana, lakini huko usiendelee na mimi sikukuita kwa sababu hiyo. Hayo yameshatokea, inabidi maisha yasonge mbele."

"Sawa babu, sasa mpaka leo mmeshajua yuko wapi?" Jerry aliuliza kimtego. Nia yake ni kutaka kujua Vayajo yuko wapi na kwa nini yupo huko?

"Hadi leo si mimi, baba yake wala mama yake anayejua yuko wapi. Ni wiki ya tatu sasa hii hatujapokea simu wala taarifa kutoka sehemu yeyote ile."

"Sasa mna uhakika na usalama wake?"

Kicheko kilimtoka mzee Mbegu kikifuatia na kikohozi. Akaiminya sigara yake ili kuizima na ikabaki kipande.

"Mimi nilijua umeshakuwa mkubwa, kumbe bado ni mdogo. Labda kama unauliza kiujanja, lakini nikwambie yule ni msichana mkubwa, na hapa alikuwa kwenye sherehe za harusi, kutoweka kwake hakuwezi kutufanya tuwe na wasiwasi. Angekuwa mdogo afadhali. Ndiyo maana niliwaambia wakwe zako hao wasiripoti tukio hili polisi kwanza, kwa sababu inaweza kuleta matatizo makubwa mbele ya safari na yeye mwenyewe binti yao akawa matatani. Yule atarudi tu, katoroka mwenyewe, hawezi kuwa yuko hatarini kwa jinsi jambo hili lilivyotokea."

"Enhee babu kuna nini, maana umeniita ujue, na mimi nimekuja kwa ajili yako tu."

"Sikiliza mjukuu wangu, haya ni maisha. Kwetu sisi mila yetu inaruhusu kabisa kuhusu hili nitakalokwambia." Mzee Mbegu alisema na kusikiliza kama ataulizwa swali, lakini Jerry akawa kama amepigwa na butwaa. Hakujua ni kitu gani tena kinataka kufanyika.

Mdomo wake ulishindwa kuuliza chochote, zaidi kwa mbali alihisi woga kumuingia. Anafahamu mila mbalimbali za makabila nchini. Hata yeye kabila lake lina utamaduni na mila zake. Nyingine ni nzuri na zimeendelezwa hadi leo kwa sababu zinaweka misingi ya kuheshimiana, kujaliana, kusaidiana na kuleta upendo na umoja.

Zipo mila ambazo si nzuri, zilizopitwa na wakati ambazo watu wa makabila yale yale pamoja na serikali wamekuwa wakizipiga vita kwa sababu zinakinzana na ustawi wa jamii ya sasa iliyoendelea.

"Kwa sababu umetoa barua, ikajibiwa, ukatoka na mahari, kila mtu anakutambua hapa na tumekuwa pamoja mpaka siku ya sherehe za harusi mambo yakaharibika. Maumivu uliyoyasikia na sisi kama wanandugu upande wa mke, tumeona tufanye kitu kimoja. Tumekutafutia mke mwingine."

**INAENDELEA JUMAPILI**



# NASLIM TZ SASA NI ZAMU YA FURAHA

MKALI wa kaswida Bongo, Naslim Tz, amewaomba wapenzi wa muziki huo kuipokea ngoma yake mpya, Furaha aliyoiachia hivi karibuni baada ya kukaa kimya kwa muda mrefu.

Akizungumza na Nipashe, Naslim amesema ndani ya muda mfupi tangu aachie kaswida hiyo, amepokea pongezi nyingi kutoka kwa mashabiki zake kwa kukata kiu yao.

"Ndugu zangu mliokuwa pamoja na mimi kutoka mwanzo mpaka sasa hivyo sina budi kuwashukuru na kuzidi kuomba sapoti kwenye video hii ya Furaha ambayo ipo tayari kwenye chaneli yangu ya YouTube ili Allah azidi kutujaza baraka," amesema Naslim.

# Mbosso aanza kukumbwa na majanga, 'Yataniua' yanyofolewa Youtube

BAADA ya mwanamuziki kutoka lebo ya WCB, Mbosso kuzindua EP yake aliyoipa jina la KHAN, jijini Dar es Salaam, nyimbo moja imeondolewa Youtube.

Ngoma iliyoondolewa iliyokuwa ikijumuisha nyimbo sita, inaitwa' YATANIUA' ambayo Mbosso ameimba na bosi wake, Diamond Platnumz, imeondolewa na kubaki tano pekee.

Nyimbo zilizobaki ni Asalaam, Wayo, Shetani, Pole na Huyu Hapa.

Tangu kuzinduliwa kwa EP hiyo, kuliibuka mjadala mkubwa kwenye mitandao ya kijamii, Diamond akituhumiwa kukopi nyimbo mbili kwenye kipande alichoimba katika wimbo huo.

Kipande cha kwanza anachodaiwa kukopi ni kutoka kwa msanii Asake wa Nigeria katika Wimbo wake wa Peace Be Unto You ambapo alichokibadilisha Diamond ni maneno tu, lakini staili ya uimbaji inafanana kwa kila kitu na kipande hicho cha Asake.

Kipande cha pili ambacho Diamond anadaiwa kukopi, ni kutoka kwenye ngoma ya Adiwele kutoka kwa msanii wa Afrika Kusini, Young Stunna akiwa amewashirikisha Kabza De Small na DJ Maphorisa.

Bado haijafahamika ni nini sababu kubwa ya kuondolewa kwa ngoma hiyo.






# Tuzo za Vyuo kutolewa Des 14

JUMLA ya wanafunzi 250 wa vyuo na vyuo vikuu wanatarajiwa kushiriki katika tamasha la kuibua vipaji na kupewa tuzo katika tamasha la vyuo mbalimbali.

Hayo yalisemwa jana jijini Dar es Salaam na katibu mkuu mtendaji wa Baraza la Sanaa Tanzania (BASATA) Kedmon Mapana, alipokuwa akizungumza na vyombo vya habari.

Alisema serikali ipo katika mkakati wa kuinua vipaji vya vijana wasomi walio mashuleni ili kuweza kuwaletea tija katika kuinua uchumi kwani kwa sasa ajira nyingi zinatokana na sanaa.

Amesema serikali kupitia Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo inajikita katika kurithisha sanaa kuongeza ubunifu na viwango katika kazi ya sanaa ikiwemo na kutoa tuzo kwa wanafunzi 42 waliofanya vizuri katika masomo yao ya sanaa.

Kwa upande wake mratibu wa tamasha hilo Shine Basili amesema tuzo hizo zinalenga vyuo vyote nchini na tayari wameshachuja washiriki mikoani na jana walianza mchakato wa kuwapata washiriki katika mkoa wa Dar es Salaam.

Amesema kilele cha tamasha hilo kinatarajiwa kufanyika Desemba 4 mwaka huu katika ukumbi wa Mwalimu Julius Nyerere jijini Dar es Salaam.

## ZISIKUPITE

### SPURS KUWAFUNGA NYOTA

MSHAMBULIAJI wa Tottenham Hotspur na nahodha wa England, Harry Kane, 29, amesitisha mazungumzo ya mkataba mpya na Spurs hadi baada ya Kombe la Dunia. Spurs pia wanataka kumpa mkataba mpya kiungo wa Denmark, Pierre-Emile Hojbjerg, 27 na mlinzi wa England, Eric Dier, 28, kwa mikataba mipya. ***(London Evening Standard)***

### KANE AWINDWA

HARRY Kane analengwa na Bayern Munich, ambao wamekosa mabao ya Robert Lewandowski, 34, tangu mshambuliaji huyo wa Poland ajiunge na Barcelona. ***(Express)***

### CONTE ATAKIWA JUVE

KLABU ya Juventus inataka kumteua kocha wa Tottenham, Antonio Conte kwa ajili ya kuanza kwa msimu wa 2023-24 baada ya mabingwa hao mara 36 wa Italia kuondolewa kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya. Mkataba wa Conte unaendelea hadi mwisho wa msimu huu na kuna chaguo kwa upande wa Spurs kuuongeza kwa mwaka mwingine. ***(Gazzetta dello Sport)***

### ATAKIWA NEWCASTLE

KLABU ya Newcastle United inavutiwa na winga wa Brazil, Eguinaldo, 18, ambaye anacheza katika daraja la pili la Brazil kwa Vasco da Gama. Kipengele cha kuachiliwa huru kwa pauni milioni 26 kimeingizwa kwenye mkataba wa mchezaji huyo. ***(Chronicle)***

### HOWE AKANUSHA

KOCHA wa Newcastle United, Eddie Howe amekanusha mazungumzo ya mkataba mpya na klabu hiyo na kiungo wao wa kati wa Paraguay, Miguel Almiron, 28, akisema wako katika kipindi chenye shughuli nyingi na mazungumzo yoyote yatafanyika hapo baadaye. ***(Sky Sports)***

### MELO KUBAKI KWA MKOPO

KIUNGO wa kati wa Juventus na Brazil, Arthur Melo, 26, atasalia kwa mkopo Liverpool kwa muda wote uliosalia licha ya kuumia vibaya paja. Melo alicheza kwa dakika 13 pekee tangu ajiunge na Wekundu hao Septemba. ***(Mirror)***

### GARNACHO AWANIWA

KLABU ya Manchester United wako kwenye mazungumzo kuhusu mkataba mpya wa muda mrefu wa winga wao wa chini ya miaka 18 raia wa Argentina, Alejandro Garnacho. ***(Fabrizio Romano on Twitter)***

### DE GEA ATEMWA

GOLIKIPA wa Manchester United, David de Gea, 31, hatahudhuria Kombe la Dunia nchini Qatar baada ya kuripotiwa kuachwa kwenye orodha ya wachezaji 55 Hispania. ***(Mail)***

### JORGINHO AITAKA BARCA

KIUNGO wa Chelsea, Jorginho, 30, atasita kufanya uamuzi wa kuondoka Stamford Bridge hadi atakapoosikia ofa kutoka kwa Barcelona. Kiungo huyo wa kati wa Italia anavutiwa na timu hiyo ya Katalunya na atapatikana bila malipo mwishoni mwa msimu huu. ***(Sport)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# PEP: MAN UNITED SASA INAREJEA

**MANCHESTER,** England

### Asema anafurahia kuona Mashetani Wekundu wakionesha ushindani na anaamini...

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola amekiri kwamba anaiona Manchester United 'hatimaye inarejea' baada ya takriban muongo mmoja wa kuhangaika kuwa na ushindani kwenye Ligi Kuu England.

**United haijashinda, au kuwa kwenye ushindani wa kuwania taji la Ligi Kuu ya England tangu Sir Alex Ferguson alipostaafu mwaka 2013.**

Katika misimu tisa kamili tangu wakati huo, wamemaliza nje ya nne bora na kushindwa kufuzu kwa Ligi ya Mabingwa Ulaya mara tano.

Mashetani Wekundu hao walimaliza wakiwa nafasi ya pili chini ya Jose Mourinho msimu wa 2017/18 na Ole Gunnar Solskjaer 2020/21.

Hata hivyo, ingawa timu yake ya City iliifunga United mabao 6-3 katika mchezo wa hivi karibuni wa dabi ya Manchester, na Guardiola amesema 'anapenda' anachokiona kwenye kipindi hiki kwa wapinzani wake chini ya Erik ten Hag.

"Ninahisi United inarejea," alisema bosi huyo wa City.

"Hatimaye United inarejea - nimeiona Alhamisi (dhidi ya Sheriff) na dhidi ya Chelsea katika kipindi cha kwanza (wikiendi iliyopita).

"Nilisema napenda ninachokiona United kwa sasa. Kutakuwa na timu nyingi kama United ikipigana. Ndiyo maana inabidi upambane ili kufuzu kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya na kupigania ubingwa."

Licha ya kuwa na msimu mzuri wa kujiandaa na msimu huu, United walianza vibaya zaidi chini ya Ten Hag Agosti wakati vipigo mfululizo dhidi ya Brighton na Brentford vilimfanya kuwa kocha wa kwanza wa klabu hiyo kupoteza michezo yake miwili ya kwanza ndani ya miaka 101.

Lakini sasa mchango wa Mholanzi huyo umeonekana tangu wakati huo, na kufanya alama yake kwenye timu, na wamepoteza pointi kidogo tu huku wakipata ushindi dhidi ya Liverpool na Arsenal.

Guardiola, ambaye alifanya kazi na Ten Hag katika klabu ya Bayern Munich, mwenyewe anajua hasa jinsi ilivyo kujaribu kujenga timu itakayoshinda mataji wakati mpya kabisa kwenye Ligi Kuu.

LIVE IN PLAY
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 389

MECHI KALI
MANCHESTER UTD
VERSUS
WEST HAM
1 | 1.73
X | 3.69
2 | 4.36

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# SIMEONE HAJALI KUKOSOLEWA



**MADRID,** Hispania

DIEGO Simeone hajali mashabiki wa Atletico Madrid wanafikiria nini juu yake baada ya kuondolewa kwao kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, akisisitiza kwamba anaangalia zadi yajayo.

Rojiblancos hao walitolewa kwenye michuano hiyo baada ya sare ya 2-2 dhidi ya Bayer Leverkusen, Jumatano, ambapo Yannick Carrasco alikosa penalti ya dakika za mwisho.

Na Simeone amesema Atletico hajishughulishi na maoni ya mashabiki wake kuhusu mustakabali wake.

"Ninahisi kwamba tunapaswa kucheza mchezo mzuri, kwamba tunapaswa kuendelea kufanya kazi na kutoa kila kitu," alisema.

"Sifikirii juu ya kitu chochote zaidi ya kile kilicho mbele yangu. 'Sijali wanachofikiria kunihusu," alisema.

Simeone anasema wachezaji wake hawapaswi kuzingatia kushindwa kwao kwa Ligi ya Mabingwa Ulaya.

"Kila kitu kinaendelea," aliongeza. "Bado nadhani timu inafanya vizuri, kutafuta kile kinachotutambulisha kwenye mchezo na kuwa na nguvu."



## Conte: Tusikae kimya kwa maamuzi mabaya

**LONDON,** England

ANTONIO Conte hataki Tottenham Hotspur "ikae kimya" kutokana na maamuzi ya hivi karibuni ambayo anahisi yameenda kinyume na timu yake.

Bosi huyo wa Spurs alikasirishwa mara mbili katika wiki iliyopita, kwanza na bao la kwanza la Newcastle United katika ushindi wa 2-1 kwenye Uwanja wa Tottenham Hotspur Jumapili iliyopita likitolewa licha ya imani ya Conte kwamba mfungaji Callum Wilson alimzuia kipa Hugo Lloris.

Kisha katika sekunde za mwisho za sare ya 1-1 Jumatano nyumbani na Sporting CP kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, bao la Harry Kane lilikataliwa kwa kuwa ameotea baada ya ukaguzi wa muda mrefu wa VAR, ambao ulimkasirisha sana Conte hadi akaonyeshwa kadi nyekundu.

"Nilizungumza na mkurugenzi wa michezo (Fabio Paratici) na pia nilituma ujumbe kwa (mwenyekiti) Daniel Levy," alisema Conte katika mkutano na waandishi wa habari juzi.

"Pia baada ya kile kilichotokea dhidi ya Newcastle, tulizungumza juu ya hili, kwa sababu kuna picha wazi sana kwamba ilikuwa faulo.

,471,330

JACKPOT
MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 01/11/22 | 20:30 | Racing Santander vs Alaves | 2.90 | 2.85 | 2.65 |
| 02. 01/11/22 | 20:45 | Porto vs Atletico Madrid | 2.38 | 3.27 | 2.83 |
| 03. 01/11/22 | 22:45 | Hull City vs Middlesbrough | 2.64 | 3.18 | 2.59 |
| 04. 01/11/22 | 22:45 | Coventry vs Blackburn | 2.41 | 3.17 | 2.87 |
| 05. 01/11/22 | 23:00 | Marseille vs Tottenham | 2.93 | 3.42 | 2.24 |
| 06. 01/11/22 | 23:00 | Sporting Lisbon vs Eintracht Frankfurt | 2.32 | 3.38 | 2.83 |
| 07. 01/11/22 | 23:00 | UD Ibiza Eivissa vs Leganes | 2.37 | 3.07 | 3.02 |
| 08. 02/11/22 | 22:45 | Birmingham vs Millwall | 2.54 | 3.19 | 2.69 |
| 09. 02/11/22 | 22:45 | Huddersfield vs Sunderland | 2.67 | 3.16 | 2.57 |
| 10. 02/11/22 | 23:00 | Mirandes vs Tenerife | 2.85 | 3.05 | 2.55 |
| 11. 03/11/22 | 20:45 | Olympiakos vs Nantes | 3.00 | 3.30 | 2.31 |
| 12. 03/11/22 | 20:45 | Zalgiris vs Slovan Bratislava | 3.04 | 3.39 | 2.24 |
| 13. 03/11/22 | 23:00 | Silkeborg vs Anderlecht | 2.36 | 3.40 | 2.85 |

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAPILI - 30/10/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:30 | 2984 | Empoli vs Atalanta | 4.16 | 3.71 | 1.75 |
| 15:00 | 1306 | AJ Auxerre vs AC Ajaccio | 2.54 | 3.04 | 2.84 |
| 15:00 | 3278 | Livingston vs Celtic | 9.98 | 5.39 | 1.27 |
| 15:00 | 5049 | HB Koge vs Sonderjyske | 2.58 | 3.46 | 2.37 |
| 15:30 | 1698 | Anderlecht vs Eupen | 1.43 | 4.57 | 6.36 |
| 16:00 | 3561 | Lyngby vs Aarhus | 2.90 | 3.44 | 2.28 |
| 16:00 | 5578 | Osasuna vs Valladolid | 1.90 | 3.40 | 4.00 |
| 16:15 | 3983 | FC Sion vs FC Zurich | 2.27 | 3.47 | 2.88 |
| 16:30 | 2402 | Twente vs Waalwick | 1.46 | 4.48 | 5.77 |
| 16:30 | 3804 | PSV Eindhoven vs NEC Nijmegen | 1.22 | 6.38 | 9.96 |
| 17:00 | 1440 | Sporting Farense vs Oliveirense | 1.57 | 3.85 | 5.33 |
| 17:00 | 1509 | Nantes vs Clermont Foot | 1.98 | 3.53 | 3.48 |
| 17:00 | 2650 | Cremonese vs Udinese | 3.82 | 3.67 | 1.83 |
| 17:00 | 2949 | Monaco vs Angers | 1.38 | 4.98 | 6.78 |
| 17:00 | 3681 | Besiktas vs Umraniyespor | 1.34 | 5.00 | 7.80 |
| 17:00 | 4028 | Brest vs Reims | 2.53 | 3.27 | 2.68 |
| 17:00 | 4584 | Rennes vs Montpellier | 1.36 | 5.00 | 7.19 |
| 17:00 | 4769 | Spezia vs Fiorentina | 3.87 | 3.53 | 1.86 |
| 17:00 | 5174 | Arsenal vs Nottingham | 1.23 | 5.69 | 10.66 |
| 17:30 | 1999 | Union Berlin vs Monchengladbach | 2.02 | 3.38 | 3.48 |
| 18:00 | 1474 | Ross County vs Hearts | 3.54 | 3.34 | 2.03 |
| 18:00 | 4250 | AEK Larnaca vs Karmiotissa | 1.46 | 4.41 | 6.22 |
| 18:15 | 2392 | Malaga vs Eibar | 3.23 | 3.08 | 2.24 |
| 18:15 | 3506 | Real Madrid vs Girona | 1.20 | 6.59 | 11.98 |
| 18:30 | 1037 | BSC Young Boys vs FC Basel | 1.63 | 3.97 | 4.77 |
| 18:30 | 2242 | Boavista vs FC Vizela | 2.44 | 3.19 | 2.84 |
| 18:30 | 2480 | Portimonense vs GD Estoril | 2.34 | 3.14 | 3.04 |
| 18:30 | 4795 | FC Winterthur vs St. Gallen | 3.43 | 3.68 | 1.95 |
| 18:45 | 2164 | AZ Alkmaar vs FC Volendam | 1.19 | 6.75 | 10.91 |
| 19:00 | 1125 | Rosenborg vs Bodo Glimt | 2.84 | 3.54 | 2.27 |
| 19:05 | 5185 | Lorient vs Nice | 2.43 | 3.22 | 2.83 |
| 19:15 | 5412 | Manchester Utd vs West Ham | 1.73 | 3.69 | 4.36 |
| 19:30 | 1383 | NK Mura vs ASK Bravo | 2.11 | 3.26 | 3.12 |
| 19:30 | 4994 | Schalke 04 vs SC Freiburg | 3.77 | 3.62 | 1.86 |
| 20:00 | 1061 | Lazio vs Salernitana | 1.47 | 4.46 | 5.75 |
| 20:00 | 1217 | Brondby vs Aalborg | 1.71 | 3.69 | 4.59 |
| 20:00 | 4076 | Istanbulspor vs Fenerbahce | 6.00 | 4.40 | 1.47 |
| 20:30 | 1117 | FC Cartagena vs Granada | 2.46 | 3.13 | 2.83 |
| 20:30 | 3768 | AEK Athens vs PAOK | 1.61 | 3.63 | 5.57 |
| 20:30 | 4000 | Athletic Bilbao vs Villarreal | 2.19 | 3.31 | 3.21 |
| 20:30 | 5271 | OH Leuven vs KAA Gent | 3.53 | 3.58 | 1.95 |
| 21:00 | 4549 | Casa Pia Atletico vs Rio Ave | 2.03 | 3.18 | 3.73 |
| 21:30 | 1781 | FC Koln vs Hoffenheim | 2.73 | 3.42 | 2.37 |
| 22:00 | 1993 | Shamrock Rovers vs Derry City | 2.08 | 3.21 | 3.25 |
| 22:45 | 1151 | Torino vs AC Milan | 3.48 | 3.23 | 2.07 |
| 22:45 | 4402 | Lyon vs Lille | 2.04 | 3.62 | 3.23 |
| 23:00 | 2601 | Charleroi vs Royal Antwerp | 3.29 | 3.53 | 2.05 |
| 23:00 | 4667 | Real Sociedad vs Betis | 2.02 | 3.41 | 3.56 |
| 23:30 | 1084 | Gil Vicente vs Sporting Braga | 4.39 | 3.64 | 1.75 |
| 23:30 | 5125 | Colo Colo vs O Higgins | 1.48 | 3.89 | 6.03 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.



# 120 WAITAKA AZAM FC

Na Hadija Mngwai

HUKU wakimtambulisha Kocha wa Viungo Mtunisia, Moadh Hiraoui, Azam FC imepokea CV za makocha 120 kutoka ndani na nje ya nchi kutaka kurithi mikoba ya Mfaransa, Denis Lavagne.

Azam imemtambulisha Hiraoui jana kuchukua mikoba ya Mikel Guillen aliyeachana na klabu hiyo hivi karibuni huku wakiendelea kusaka kocha mkuu kuchukua mikoba ya Denis Lavagne aliyedumu mwezi mmoja ndani ya kikosi hicho.

**Hiraoui ambaye tayari ameshaanza kuitumikia timu hiyo, aliwahi kuzitumikia Esperance ya Tunisia na Al Hilal ya Sudan ambapo pia ana PhD ya Sayansi ya Michezo na Afya.**

Kocha huyo amesaini mkataba wa mwaka mmoja wa kuitumikia timu hiyo huku ikiwa na kipengele cha kuongeza, amewahi pia kufanya kazi katika timu ya Dibba Al Hisn na Hajer FC ya Saudi Arabia.

Akizungumza na Nipashe, Kaimu Ofisa Habari wa Azam, Hashimu Ibwe amesema kuwa, baada ya kumshusha kocha huyo wa viungo kutoka Tunisia pia wakati wowote kuanzia sasa watamtangaza kocha mkuu ambapo wameshapokea CV za makocha 120 wanaotaka kutua klabuni hapo.

"Tumeshamaliza suala la kocha wa viungo sasa tupo katika mchakato wa kumpata kocha mkuu kwa sasa timu inaendelea kuwa chini ya kocha Kali Ongala.

"Tumepokea CV za makocha 120 kutoka ndani na nje ya nchi wote wakihitaji kufundisha Azam kwa sasa tupo katika mchakato wa kuangalia nani anafaa kuiongoza timu," alisema Ibwe.



Kikosi cha Simba Queens kikifanya mazoezi kwenye Uwanja wa Akademi ya Fusi kwa ajili ya kujiandaa na mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwa Wanawake dhidi ya ASFAR FC itakayochezwa leo jijini Rabat, Morocco. **PICHA: SOMOE NG'ITU**

# *Yanga yazidi kupaa*

INATOKA UK. 24

Kikosi cha Simba kinashuka dimbani kikiwa na kumbukumbu ya kupoteza mchezo uliopita kwa kukubali kichapo cha bao 1-0 kutoka kwa Azam FC. Simba itamkosa nyota wake Nelson Okwa ambaye ni majeruhi, huku Shomari Kapombe akiwa amerejea mazoezini akiendelea kujifua katika uangalizi wa madaktari wa timu hiyo.

Habari njema kwa mashabiki wa Simba ni kurejea uwanjani kwa Israel Mwenda ambaye amepona na kurejea mazoezini huku kiungo Mzamiru Yassin aliyemaliza adhabu yake ya kadi tatu za njano na aliyekosa mechi iliyopita na Azam na leo atakuwepo katika kikosi cha Wekundu hao wa Msimbazi.

Kwa upande wa Mtibwa Sugar wametoka kupata pointi tatu ugenini kwa ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Dodoma jiji FC wiki iliyopita.

Kocha wa Simba, Juma Mgunda amesema mechi hiyo ni muhimu kwa kila timu na wamejiandaa vizuri tayari kwa ajili ya mchezo wao wa leo.

Alisema mbali na nyota hao wawili Okwa na Mwanuke ambao wako katika matibabu hawana majeruhi, wengine wakiendelea vizuri na suala la kucheza hilo litakuwa ni mipango yake.

# Simba Queens

INATOKA UK. 24


anaonyesha ana nia ya kufanya vyema huku akifurahishwa na ushindani walioonyesha katika mazoezi kuanzia walipokuwa Dar es Salaam hadi Rabat ambapo timu za Kundi A zinacheza mechi zake za awali.

Nahodha wa Simba Queens, Fatma Issa "Fetty Densa", aliliambia gazeti hili wachezaji wote wana morali ya hali ya juu ya kuhakikisha wanapambana kusaka ushindi.

Beki huyo alisema wanataka kuwapa furaha Watanzania na wanajua kiu ya mafanikio ambayo wanadaiwa na mashabiki wa kandanda walioko Tanzania.

# Michezo

Jumapili Oktoba 30, 2022
Nipashe



Pep: Man Utd sasa inarejea UKURASA 21



Nahodha wa Yanga, Feisal Salum 'Fei Toto' (kushoto) akijiandaa kumtoka mlinzi wa Geita Gold FC wakati wa mchezo wa Ligi Kuu Tanzania bara baina ya timu hizo jana kwenye uwanja wa CCM Kirumba, Mwanza. Yanga ilishinda bao 1-0. **PICHA: YANGA**

## Simba Queens karata ya kwanza Morocco

**Na Somoe Ng'itu,** RABAT

TIMU kutoka Tanzania, Simba Queens inatarajia kuweka historia ya kushiriki kwa mara ya kwanza Fainali za Ligi ya Mabingwa Afrika kwa Wanawake itakapokutana na wenyeji ASFAR FC katika mechi ya ufunguzi itakayochezwa leo kuanzia saa 4:00 usiku kwenye Uwanja wa Prince Heritier Moulay El Hassan uliopo jijini hapa.

Simba Queens inashiriki fainali hizi baada ya kutwaa ubingwa wa Afrika Mashariki na Kati katika michuano iliyopita Agosti mwaka huu jijini, Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Simba Queens, Charles Lukula, alisema kikosi chake kimejiandaa vizuri kushiriki mashindano haya na anaamini watafanya vyema na kusonga mbele.

Lukula alisema anaheshimu kila timu iliyokata tiketi ya kushiriki fainali hizi, hivyo amewaandaa wachezaji wake kucheza katika kiwango cha juu ili watimize malengo yaliyowaleta na si vinginevyo.

Kocha huyo alisema wamejiandaa kukutana na changamoto mbalimbali kwa sababu kila mechi wanatarajia itakuwa na ushindani kutokana na wote kuhitaji kucheza hatua inayofuata ya nusu fainali.

"Tumepata video za mechi zao, tumeyafanyia kazi mapungufu yao na kujipanga kuwakabili katika idara ambazo wako imara, nimewaambia wachezaji wangu wawe na utulivu kila wanapokuwa na mpira lakini pia wasiwape nafasi wapinzani kumiliki mpira muda mrefu," alisema Lukula.

Aliongeza kila mchezaji

INAENDELEA UK. 23

# YANGA YAZIDI KUPAA

### Yafikisha mechi 45 bila kufungwa, Simba hasira...

**Adam Fungamwango na Saada Akida**

BAO la mkwaju wa penalti lililowekwa wavuni na Mghana Bernard Morrison, liliiwezesha Yanga kujiongezea pointi kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, ikiichapa Geita Gold bao 1-0 jana jioni kwenye Uwanja wa CCM Kirumba ,Mwanza.

**Hiyo ilikuwa ni mechi ya 45 kwa Yanga bila kupoteza tangu ilipofanya hivyo mara ya mwisho Aprili 25, 2021, ilipochapwa bao 1-0 na Azam FC kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa kwa bao ya Prince Dube, ikiwa ni mechi ya Ligi Kuu msimu uliopita.**

Ushindi huo wa Yanga umemaliza rekodi ya Geita Gold ya kucheza mechi nne mfululizo bila kupoteza tangu ilipofungwa bao 1-0 na Dodoma Jiji, Septemba 29 mwaka huu.

Baada ya hapo ilicheza mechi nne mfululizo bila kupoteza, ikishinda tatu na suluhu moja dhidi ya Coastal Union, Oktoba 13.

Ni mechi ambayo pia imezima ndoto za mchezaji wa zamani wa Yanga ambaye kwa sasa anaichezea Geita Gold, Saido Ntibazonkiza kufunga bao kwenye mechi ya tatu mfululizo baada ya kufanya hivyo kwenye mechi mbili zilizopita dhidi ya Namungo, Oktoba 22 na Ruvu Shooting Oktoba 25, akifunga bao moja kila mchezo, timu yake ikishinda mabao 2-1 kwenye mechi zote mbili.

Kwenye mechi ya jana alicheza vema, lakini alikumbana na upinzani mkali kutoka kwa wachezaji wa Yanga ambao walikuwa wakimlinda asilete madhara kwa njia yoyote ile. Yanga iliandika bao pekee dakika ya 45 lililofungwa kwa mkwaju wa penalti, baada ya mlinzi George Wawa kuunawa mpira kwenye eneo la hatari na Morrison akakwamisha wavuni.

Hata hivyo, kwenye picha za marejeo zilionyesha aliushika akiwa nje kidogo ya eneo ya hatari.

Yanga ilianza pambano hilo kwa kasi kwani dakika ya tano tu ilifanya shambulizi kali ambalo nusura lizae bao, kwani mpira wa faulo wa haraka wa Denis Nkane ulienda kwa Aboubakar Salum 'Sure Boy' ambaye aliachia shuti kali, lakini kipa wa Geita Gold Mrundi MacArthur Arakaza alikuwa makini akaruka na kuupangua mpira huo pembeni, lakini haukutoka, ukarudishwa tena ndani, safari hii ukimkuta mkali wa mashuti, Feisal Salum 'Fei Toto', alitandika kombora kali lililotoka nje kidogo ya lango.

Dakika mbili tu baadaye Fei Toto alipiga tena hodi langoni mwa Geita Gold, akiwa nje kidogo ya eneo la hatari aliachia shuti kali lililompita kipa, lakini badala ya kujaa wavuni ukagonga mwamba wa juu na kurejea uwanjani, ikawa manusura kwa wenyeji.

Kipindi cha pili timu zote zilifanya mabadiliko na mpira ukachangamka zaidi, lakini hakukuwa na bao lolote.

Hata hivyo, sifa kubwa zimwendee kipa Arakaza ambaye alikuwa shujaa kwa kuokoa hatari nyingi ikiwemo kichwa kilichopigwa na Fiston Mayele dakika ya 73 akiunganisha krosi na Fei Toto, lakini akaruka juu na kuupiga ngumi mpira ukatoka juu ya lango huku mashabiki wa Yanga wakiwa wamenyanyuka. Aliingia kuchukua nafasi ya Makambo.

Ni matokeo yanayoifanya Yanga kuendelea kuwa kileleni, sasa ikifikisha pointi 20, huku Geita Gold ikiwa kwenye nafasi ya tisa na pointi zake 13

Wakati huo huo, Simba leo inashuka dimbani ikiwa na kibarua kigumu kwenye mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Mtibwa Sugar, Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam majira ya saa 1:00 usiku.

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >